Tangazo la Serikali Na 162 la tarehe 27/4/2017

SHERIA YA FEDHA ZA SERIKALI ZA MITAA
(SURA 290)

# SHERIA NDOGO

*Zimetungwa chini ya kifungu cha 7 (1) na 16 (1)*

SHERIA NDOGO ZA (ADA NA USHURU) ZA HALMASHAURI YA WILAYA YA MKURANGA 2018

Jina na mwanzo wa kutumika

1. Sheria Ndogo hizi zitajulikana kama Sheria Ndogo za ( Ada na Ushuru) za Halmashauri ya Wilaya ya Mkuranga za mwaka 2018 na zitaanza kutumika baada ya kutangazwa kwenye Gazeti la Serikali.

Matumizi

2. Sheria Ndogo hizi zitatumika katika eneo lote la Halmashauri ya Wilaya ya Mkuranga.

Tafsiri

3. Katika Sheria Ndogo hizi isipokuwa pale itakapoelezwa vinginevyo;

"Ada na Ushuru" maana yake ni malipo yanayolipwa kwa Halmashauri au wakala wake kwa ajili ya huduma, vibali, au leseni mbalimbali zitolewazo na Halmashauri;

"Afisa Mwidhiniwa" Maana yake ni Afisa yeyote wa Halmashauri aliyeteuliwa na Mkurugenzi kusimamia utekelezaji wa Sheria Ndogo hizi.

"Chombo cha usafiri" maana yake ni chombo chochote kinachotumika kusafirishia mtu,watu au mizigo kutoka sehemu moja kwenda sehemu nyingine isipokuwa mkokoteni au wanyama wanaotumika kama kusafirisha watu au mizigo.

"Halmashauri" Maana yake ni Halmashauri ya Wilaya ya

Mkuranga.

"Kibali" maana yake ni idhini au ruhusa ya maandishi inayotolewa na Halmashauri.

Kituo cha mabasi" maana yake ni eneo maalum lililotengwa na Halmashauri kwa madhumuni ya kupakia na kuteremshia abiria na mizigo.

"Madini ya Ujenzi" maana yake ni mawe, kokoto, tarazo, udongo, kifusi, mchanga na chokaa.

"Machinjio" maana yake ni sehemu iliyotengwa na Halmashauri kwa ajili ya kuchinjia wanyama na kuanika ngozi.

"Mkurugenzi" Maana yake ni Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Mkuranga na ni pamoja na Afisa yeyote atakayeteuliwa kukaimu nafasi ya Mkurugenzi.

"Utamaduni" maana yake ni sanaa za maonyesho, sanaa za ufundi, muziki wa asili, michezo, muziki wa dansi, video, muziki wa taarabu, maonyesho ya sinema,mazingaombwe, tiba za jadi na matumizi ya viwanja vya michezo.

"Usajiri wa vyombo vya usafiri" maana yake ni utaratibu utakaowekwa na Halmashauri wa kuorodhesha idadi ya vyombo vya usafiri vinavyofanya biashara ndani ya eneo la Halmashauri.

Wakala" maana yake ni Mtu, Taasisi, Kampuni au asasi yoyote iliyoteuliwa na Halmashauri kukusanya mapato kwa niaba ya Halmashauri chini ya kifungu cha 31 cha Sheria ya Fedha ya Serikali za Mitaa.

Ada na Ushuru

4.-(1). Halmashauri itaanzisha na kutoza Ada na Ushuru kwa huduma na shughuli mbalimbali kama zilivyoonyeshwa kwenye Jedwali la kwanza la Sheria Ndogo hizi.

(2) Ushuru utakaotozwa chini ya Sheria Ndogo hizi unapaswa kulipwa kabla ya huduma kutolewa.

(3) Huduma zitakazotozwa Ada na Ushuru katika Sheria Ndogo hizi ni:-

(a) Ushuru wa mifugo iliyounzwa mnadani;
(b) Ushuru wa machinjio na ukaguzi wa nyama;
(c) Huduma ya tiba za asili na uuzaji wa dawa za jadi;

(d) Vibali vya sanaa burudani na michezo;
(e) Ushuru wa kuegesha magari katika magulio na masoko ya minada;
(f) Ushuru katika masoko na magulio;
(g) Ushuru wa Mazao ya misitu;
(h) Ushuru wa Mazao ya kilimo;
(i) Madini ya ujenzi;
(j) Usajiri wa vyombo vya usafiri;
(k) Ukaguzi wa kiafya;
(l) Vibali vya ujenzi;
(m) Ushuru wa kituo cha mabasi;
(n) Ushuru mwingine;

Wajibu wa kulipa Ada na Ushuru

5.-(1) Itakuwa ni wajibu wa kila mtu anayestahili kulipa Ada au Ushuru kulipa Ada au Ushuru kama ilivyoelekezwa kwenye jedwali la Sheria Ndogo hizi.

(2) Itakuwa ni wajibu wa kila mtu anayetakiwa kulipa Ada na Ushuru kuwa kuhakikisha anapewa stakabadhi kwa malipo aliyoyafanya.

Msamaha wa kodi

6. Mtu yeyote ambaye atakuwa anafanya shughuli zilizoorodheshwa katika jedwali la Sheria Ndogo hizi atasamehewa Ada na Ushuru iwapo shughuli ambayo atakuwa anaifanya itakuwa si ya faida hata hivyo shughuli hiyo itatakiwa itambulike kisheria kama ni shughuli isiyo na faida kutokana na usajili au kibali cha taasisi au shughuli ya mtu huyo.

Shughuli kutokuwa ya faida

7. Bila kuathiri kifungu cha 6 cha Sheria Ndogo hizi, shughuli itakayosamehewa kulipa Ada na Ushuru kwa kigezo cha kutokuwa ya faida itatakiwa itambulike kutokana na usajili au kibali cha shughuli hiyo.

Wajibu wa Afisa Mwidhiniwa

8. Afisa Mwidhiniwa atakuwa na mamlaka ya kufanya ukaguzi kwa shughuli yoyote iliyotajwa na Sheria Ndogo hizi kwa lengo la kuona kama Sheria Ndogo hizi zinatekelezwa.

Mamlaka ya Mkurugenzi

9. Mkurugenzi atakuwa na mamlaka ya kudai Ada na Ushuru ndani ya siku 14 iwapo ada au ushuru huo utakua haujalipwa katika muda uliokubaliwa na kama mdaiwa hatalipa ndani ya siku hizo, Mkurugenzi atadai ushuru huo kwa njia ya mahamaka.

Uteuzi wa

10. Halmashauri inaweza kumteua kwa maandishi mtu

Wakala

yeyote, Taasisi au Kampuni kuwa wakala wa kukusanya Ushuru kwa niaba ya Halmashauri.

Wajibu wa Wakala

11. Wakala atakayeteuliwa chini ya kifungu cha 10 cha Sheria Ndogo hizi atakuwa na wajibu wa:

(a) kutoa taarifa ya maandishi juu ya majina au orodha ya watu wanaotakiwa kutozwa ushuru au ada ndani ya eneo au sehemu ya eneo ambapo ameteuliwa kukusanya ushuru.

(b) kukusanya na kupokea ada na ushuru kutoka kwa kila mtu anayedaiwa ada na ushuru chini ya Sheria Ndogo hizi.

(c) kuwasilisha pesa alizokusanya kwa Halmashauri kwa mujibu wa mkataba;

(d) kuwasilisha kwa Halmashauri taarifa ya jina la mtu yeyote atakayeshindwa kulipa kiasi cha deni analodaiwa kwa ajili ya ada au ushuru wowote aliotozwa chini ya Sheria Ndogo hizi

Makosa kwa Wakala

12. Wakala yeyote aliyeteuliwa atakuwa ametenda kosa chini ya Sheria Ndogo hizi ikiwa:

(a) atashindwa kuwasilisha Halmashauri fedha za Ada au Ushuru alizokusanya;

(b) atamtoza mtu yeyote kiasi cha Ada au Ushuru zaidi ya kile kilichowekwa chini ya Sheria Ndogo hizi;

(c) atatoa taarifa za uongo kwa mdomo au kwa maandishi juu ya idadi ya walipa ushuru au kiasi cha ada au ushuru alichokusanya au alichopokea; au

(d) atashindwa kutekeleza wajibu kama wakala chini ya Sheria Ndogo hizi;

Makosa

13. Itakuwa ni kosa kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi endapo mtu yeyote:-

a) atashindwa, atadharau, au atakataa kulipa Ada au Ushuru au kutekeleza agizo lolote alilopewa na Halmashauri kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi;

b) atamshawishi mtu au kundi la watu kukataa au kukwepa kulipa Ada na Ushuru;

c) atamzuia kwa namna yeyote ile Afisa Mwidhiniwa kutekeleza majukumu yake kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi;

d) atatumia nyaraka za kughushi kwa nia ya kujipatia manufaa yatokanayo na ukusanyaji wa Ada na Ushuru ndani ya Halmashauri;

e) atashindwa au atatoa taarifa za uongo kwa Halmashauri au Wakala kuhusu bidhaa au mali zinazotakiwa kulipiwa ada au ushuru,au atashindwa kutoa taarifa zinazotakiwa na Halmashauri;

f) atashindwa kutunza Kumbukumbu sahihi, za malipo ya ada au ushuru;

Adhabu

14. Mtu yeyote atakayekwenda kinyume na masharti ya Sheria Ndogo hizi atakuwa ametenda kosa na akipatikana na hatia atatozwa faini isiyopungua shilingi laki mbili (200,000/=) na isiyozidi shilingi milioni moja (1,000,000/=) au kifungo kisichopungua miezi kumi na mbili (12) na kisichozidi miaka miwili (2) au adhabu zote mbili kwa pamoja yaani faini na kifungo.

Kufifilisha kosa

15. Mkurugenzi anaweza kumtoza mtu yeyote faini isiyopungua shilingi laki mbili (200,000/=) na isiyozidi shilingi laki tano (500,000/=) iwapo mkosaji atakiri kosa kwa hiari yake kwa maandishi na kukubali kutekeleza wajibu wake pamoja na kulipa faini anayodaiwa kwa kujaza fomu maalum kama ilivyoelekezwa katika jedwali la pili la Sheria Ndogo hizi.

Kufutwa kwa Sheria Ndogo GN 366/2010

16. Sheria Ndogo za (Ada na Ushuru) za Halmashauri ya Wilaya ya Mkuranga GN. Na 366/ 2010 zinafutwa.

*JEDWALI LA KWANZA*

Limetungwa chini ya kifungu cha 4 (1)

SEHEMU I

USHURU WA MIFUGO ILIYOUNZWA (MNADANI)

| AINA YA MFUGO | KIWANGO |
|---|---|
| (i) Ngo'mbe | Shilingi 5000 kwa kila mmoja |
| (ii) Mbuzi/Kondoo | Shilingi 1500 kwa kila mmoja |
| (iii) Nguruwe | Shilingi 3000 kwa kila mmoja |
| (iv) kuku /kanga/bata | Shilingi 300 kwa kila mmoja |

SEHEMU YA II

USHURU WA MACHINJIO NA UKAGUZI WA NYAMA

| Na | AINA MFUGO | USHURU WA MACHINJIO (Tshs) | ADA YA UKAGUZI WA NYAMA (Tsh) |
|---|---|---|---|
| 1 | Ngo'mbe | 4000/= kila mmoja | 2000/= kila mmoja |
| 2 | Mbuzi/Kondoo | 1000/= Kila mmoja | 1000/= kila mmoja |
| 3 | Nguruwe | 4000/= kila mmoja | 2000/= kila mmoja |
| | | | |

## SEHEMU III

## USHURU KWA WATOAJI HUDUMA YA TIBA ASILI NA WAUZAJI WA DAWA ZA JADI

| Na | KIBALI KWA MTOA HUDUMA | ADA KWA MWAKA Tshs |
|---|---|---|
| 1 | Waganga wa jadi | 35,000/= |
| 2 | Taasisi | 35,000/= |
| 3 | Wauzaji wa dawa za asili/jadi | 35,000/= |
| 4 | Kibali cha kuuza dawa za asili | 20,000/= KWA SIKU |

## SEHEMU IV
## USHURU WA VIBALI VYA SANAA, BURUDANI NA MICHEZO

| Na | AINA YA BURUDANI, SANAA, MICHEZO | ADA KWA SIKU Tshs |
|---|---|---|
| 1 | Muziki, sanaa za maonyesho, ngumi na mazingaombwe | 20,000/= kwa siku |
| 2 | Ngoma au Sherehe nyumbani | 10,000/= kwa siku |
| 3 | Huduma za kazi za sanaa kwenye kumbi zinazokidhi vigezo | 30,000/= kwa siku |
| 4 | Kibali cha michezo mbalimbali kama vile snuka,pool table,na fete | 60,000/= kwa mwaka |
| 5 | Kibali cha kuuza au kukodisha kanda za filamu au kazi nyingine za sanaa. | 40,000/=kwa mwaka |
| 6 | Kibali cha kutoa huduma ya tiba asilia na tiba mbadala. | 30,000/=kwa tukio |
| 7 | Usajili wa vikundi vya sanaa na utamaduni. | 25% ya malipo ya BASATA |
| 8 | Kibali cha kutengeneza au kurekodi kazi za sanaa. | 40,000/= kwa tukio |
| 9 | Kibali cha kutembelea maeneo ya kihistoria na kufanya utalii wa kiutamaduni. | 10,000/=kwa tukio (Watalii wa ndani)<br>20,000/=kwa tukio (Watalii wa Nje) |
| 10 | Kibali cha filamu na picha jengefu. | 60,000/= kwa mwaka |
| 11 | Utafiti wa kimafunzo. | 2,000/=kwa Mtanzania<br>100,000/=kwa mtu toka nje ya nchi |

### SEHEMU V
### USHURU WA KUEGESHA MAGARI YANAYOINGIA KATIKA MAGULIO, MASOKO NA MINADA

| Na | AINA YA MAGARI | USHURU KWA SIKU TSH. |
|---|---|---|
| 1 | Magari madogo (hiace | 1500/= |
| 2 | Taxi | 1000/= |
| 3 | Pikipiki | 500/= |
| 4 | Magari binafsi yasiyo ya biashara | 500/= |
| 5 | Gari dogo la mizigo (lori au pick- up chini ya tani 7) | 2,000/= |
| 6 | Gari kubwa la mizigo zaidi ya tani 7 | 2,500/= |

### SEHEMU VI
### USHURU KATIKA MASOKO NA MAGULIO

| NA | AINA YA BIASHARA | USHURU |
|---|---|---|
| 1 | Biashara ya nguo za mitumba | 1,000/= Kwa siku |
| 2 | Biashara ya nguo za madukani | 1,000/= Kwa siku |
| 3 | Biashara ya viatu vya mitumba | 1,000/= Kwa siku |
| 4 | Biashara ya mama lishe | 1,000/= Kwa siku |
| 5 | Biashara ya vileo | 2,000/= Kwa siku |
| 6 | Biashara ya kuchoma nyama | 2,000/= Kwa siku |
| 7 | Michezo mbalimbali katika soko | 2,000/= Kwa siku |
| 8 | Biashara za bidhaa za urembo | 1,000/= Kwa siku |
| 9 | Biashara ya vyombo vya ndani | 1,000/= Kwa siku |
| 10 | Biashara ya samaki mbalimbali | 1,000/= Kwa siku |
| 11 | Biashara nyingine | 1,000/= Kwa siku |
| 12 | | |

### SEHEMU VII
### USHURU MAZAO YA MISITU

| NA | AINA | KIWANGO (TSH.) |
|---|---|---|
| 1 | MKAA | 5% ya bei ya mauzo ya shambani |
| 2 | MBAO | 5% ya bei ya mauzo ya shambani |
| 3 | KUNI | 5% ya bei ya mauzo ya shambani |
| 4 | NGUZO | 5% ya bei ya mauzo ya shambani |
| 5 | GOGO | 5% ya bei ya mauzo ya shambani |
| 6 | FITO | 5% ya bei ya mauzo ya shambani |
| 7 | Asali | 5% ya bei ya mauzo ya shambani |
| 8 | Nta | 5% ya bei ya mauzo ya shambani |
| 9 | Kibali cha kukata mti au kuvuna mti | 10% ya thamani au bei ya mti |
| 10 | Mazao mengine ya misitu | 5% ya thamani ya zao |

## SEHEMU YA VIII

## USHURU MAZAO YA KILIMO

| NA | AINA | KIWANGO (TSH.) |
|---|---|---|
| 1 | Mpunga | 3% ya bei ya kununulia |
| 2 | Maharage | 3% ya bei ya kununulia |
| 3 | Mahindi | 3% ya bei ya kununulia |
| 4 | Ufuta | 3% ya bei ya kununulia |
| 5 | Matikiti | 3% ya bei ya kununulia |
| 6 | Mtama | 3% ya bei ya kununulia |
| 7 | Mazao mengine | 3% ya bei ya kununulia |
| 8 | Korosho | 3% ya bei ya kununulia |
| 9 | Nazi | 3% ya bei ya kununulia |
| 10 | Muhogo | 3% ya bei ya kununulia |

## SEHEMU IX

## ADA /USHURU WA MADINI YA UJENZI

| NA | AINA | KIWANGO (TSH.) |
|---|---|---|
| 1 | Maombi ya kibali cha kumiliki eneo la kuchimba madini ujenzi | (1) Mchanga 8,000,000.00<br>(2) Kokoto 1,000,000.00<br>(3) Udongo/kifusi 1,000,000.00 |
| 2 | **Ushuru kwa madini yafuatayo:** | |
| | (a) Tarazo | 3,000/= kwa tani |
| | (b) Mawe | 3,000/= kwa tani |
| | (c) Moramu | 2,000/= kwa tani |
| | (d) Kokoto | 3,000/= kwa tani |
| | (e) Udongo /kifusi | 1,000/= kwa tani |
| | (f) Mchanga | 2,000/= kwa tani |
| | (g) Madini mengine | 5,000/= kwa tani |

## SEHEMU YA X
## ADA YA USAJILI WA VYOMBO VYA USAFIRI

| NA | AINA YA CHOMBO | KIWANGO (TSH) |
|---|---|---|
| 1 | Pikipiki ya Matairi mawili na Matairi matatu | 22,000/= kwa mwaka |

## SEHEMU YA XI
## ADA ZA UKAGUZI WA KIAFYA

| Na | AINA | KIWANGO TSH |
|---|---|---|
| 1 | Nyumba za starehe (baa, vilabu vya pombe za kienyeji na nyumba ya kulala wageni | 7,000/=kila baada ya miezi sita |
| 2 | Maduka ya bidhaa | 4,000/= kila baada ya miezi sita |
| 3 | Nyumba za kutengeneza na kuuziwa vyakula na nyama choma | 5,000/= kila baada ya miezi sita |
| 4 | Ukaguzi kwa maombi ya kufungua biashara | 10,000/= |
| 5 | Ukaguzi kwa maombi ya kufungua biashara baada ya ukaguzi ili kufunguliwa upya | 10,000/= |
| 6 | Ukaguzi wa viwanda vikubwa | 100,000/= kwa mwaka |
| 7 | Ukaguzi wa viwanda vya kati | 50,000/= kwa mwaka |
| 8 | Ukaguzi wa viwanda vidogo | 20,000/= kwa mwaka |
| 9 | Ukaguzi wa wahudumu wa vyakula | 5,000/= kwa mwaka |

## SEHEMU XII
## VIBALI VYA UJENZI (BUILDING PERMITS)

| NA | AINA | KIWANGO TSH |
|---|---|---|
| **(a)** | **Ada ya idhini ya ujenzi** | |
| (i) | Ghorofa 2 na zaidi | 200,000/= |
| (ii) | Ghorofa moja | 100,000/= |
| (iii) | Nyumba ya kulala wageni | 100,000/= |
| (iv) | Kituo cha mafuta | 150,000/= |
| (v) | Nyumba ya makazi na biashara | 50,000/= |
| (vi) | Nyumba ya makazi | 30,000/= |
| (vii) | Ofisi binafsi,shule binafsi na hospitali/ zahanati binafsi | 150,000/= |
| (viii) | Maghala na bohari | 150,000/= |
| (ix) | Shopping malls na Hoteli kubwa | 300,000/= |
| (x) | Uzio | 50,000/= |
| (xi) | Majengo mengine ambayo hayajatajwa hapo juu | 30,000/= |
| **(b)** | **Ada ya mabadiliko ( alteration ) ya nyumba / jengo lilipo** | |
| (i) | Nyumba ya makazi | 20,000/= |

| | | |
|---|---|---|
| (ii) | Nyumba ya biashara | 50,000/= |
| (iii) | Ghorofa | 150,000/= |
| (iv) | Kiwanda, bohari, ghala | 150,000/= |
| **( c) Ada ya mabadiliko ya matumizi ya ardhi** | | |
| (i) | thamani ya eneo husika | 10% |

SEHEMU YA XIII
USHURU WA KITUO CHA MABASI

| Na. | AINA YA GARI | KIWANGO |
|---|---|---|
| a | Kwa gari kubwa (basi) kila linapoingia kituoni | 3,000/= |
| b | Kwa magari madogo ( hiace, tax) | 1,000/= kwa siku |
| c | Pikipiki | 500/= kwa siku |
| d | Kwa basi saizi ya kati (coaster) | 1,500/= kwa siku |

SEHEMU XIV
USHURU MWINGINE

| NA | AINA | KIWANGO TSH |
|---|---|---|
| 1. | Ushuru wa chumvi | 6,000/= kwa tani |
| 2. | Ushuru wa mnada wa jumla wa kitu kinachonadiwa | 3% ya bei ya mnada |
| 3. | Choo cha umma cha kulipia | 200/= |
| 4. | Ushuru wa nyumba za kulala wageni (Guest House levy) | 10% ya bei ya kitanda kwa usiku mmoja |
| 5. | Ada ya maombi ya zabuni | 100,000/= hadi 200,000/= kwa kila moja |
| 6. | Ada ya kukodi ukumbi wa Halmashauri | Ukumbi mkubwa 300,000/= kwa siku<br>Ukumbi mdogo 200,000/= kwa siku |
| 7. | Taasisi au mtu yeyote atakayefanya biashara ya kuuza viwanja kupitia Halmashauri atalipa: | Asilimia kumi ya thamani ya viwanja (10%)<br>20,000/= kwa fomu ya maombi |
| 8. | **USHURU WA NGOZI**<br>1. ngozi ya ng'ombe<br>2. Mbuzi, kondoo | <br>2,000/= kwa kila ngozi<br>1,000/= kwa kila ngozi |
| 9. | Ushuru wa vizimba sokoni kwa kila kizimba | 10,000/= kwa mwezi |
| 10. | **ADA YA PANGO LA VIBANDA SOKONI**<br>1. Vibanda vya duka upande wa ndani na nje ya soko<br>2. Vibanda vya biashara nyingine yoyote | 100,000/=Kwa mwezi<br>100,000/= kwa mwezi |

| | | |
|---|---|---|
| 11. | Mchoro wa mpango mji utalipiwa 10% ya gharama ya kazi zihusuzo shughuli za huduma za uandaaji wa mchoro wa mipango miji. | 10% ya gharama ya uandaaji wa michoro ya mipango miji. |
| 12. | Ujenzi wowote unaofanywa bila ya kibali utalipiwa 2% ya thamani ya maendelezo ya ujenzi huo | 2% ya thamani ya maendelezo ya ujenzi huo |
| 13. | Mawe (Beacons) | 10,000/= Kwa jiwe |
| 14. | Upimaji na ramani | 10% ya gharama za upimaji |
| 15. | Uthamini | 10% ya gharama za uthamini |
| 16. | Mabwawa ya ufugaji wa samaki,kamba, na mabirika ya chumvi | 100,000/= kwa mwaka |

**JEDWALI LA PILI**
*(Chini ya Kifungu cha 15)*

HATI YA KUKIRI KOSA

Mimi
.................................................................................................nakiri kwa hiari yangu mwenyewe mbele ya
.........................................................................................................

Ambaye ni Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Mkuranga. Kwamba, mnamo tarehe............... ya mwezi.......................mwaka.......................... nilitenda kosa la kukiuka masharti ya Kifungu cha ..............................cha Sheria Ndogo za (Ada na Ushuru) za Halmashauri ya Wilaya ya Mkuranga za mwaka 2018.

Kwa Mamlaka aliyopewa Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Mkuranga kwa hiyari yangu niko tayari kulipa kiasi cha Ada au Ushuru unaodaiwa pamoja na faini.

Nathibitisha maelezo hapo juu ni ya kweli na nimeyatoa kwa hiari yangu na ufahamu wangu.

Leo tarehe.........ya mwezi.....................mwaka......................
Jina..................................
Saini..................................

Mbele ya:
Jina.....................................
Cheo..................................
Saini...................................

Muhuri wa Halmashauri ya Wilaya ya Mkuranga ulibandikwa kwenye Sheria Ndogo hizi kwa kufuata azimio lililopitishwa kwenye Mkutano wa Halmashauri uliofanyika mnamo tarehe 15 mwezi 03 mwaka 2017 na nembo hio ilibandikwa mbele ya:-

MSHAMU A MUNDE,
*Mkurugenzi wa Halmashauri Mkuranga*

L.S

JUMA A. ABEID,
*Mwenyekiti wa Halmashauri Mkuranga*

NAKUBALI

DODOMA,
29 Machi, 2018

SELEMANI S. JAFO (MB),
*Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais,*
*TAMISEMI*

TANGAZO LA SERIKALI NA. 606 la tarehe 23/7/2021

SHERIA YA SERIKALI ZA MITAA (MAMLAKA YA WILAYA)

(SURA YA 287)

# SHERIA NDOGO

*(Imetungwa chini ya Kifungu cha 153)*

SHERIA NDOGO YA UDHIBITI WA UJENZI HOLELA YA HALMASHAURI YA WILAYA YA MKURANGA ZA MWAKA 2021.

Jina

1. Sheria Ndogo hii itajulikana kama Sheria Ndogo ya Uthibiti wa Ujenzi Holela ya Halmashauri ya Wilaya ya Mkuranga ya mwaka 2021.

Eneo la matumizi

2. Sheria Ndogo hii itatumika katika eneo lote lililo chini ya mamlaka ya Halmashauri ya Wilaya ya Mkuranga.

Tafsiri

3. Katika Sheria Ndogo hii isipokuwa pale itakapoelekezwa vinginevyo:-

"Halmashauri" maana yake ni Halmashauri ya Wilaya ya Mkuranga.

"jengo"ina maana ya nyumba, kibanda, kontena na makambi (camp site)"

"Mkurugenzi" maana yake ni Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya au Afisa yeyote wa Halmashauri atakayetekeleza au kukaimishwa majukumu ya Mkurugenzi.

"mpango wa ujenzi" ina maana ya mpango wa ujenzi ulioandaliwa na Halmashauri unaolekeza namna ya ujenzi katika maeneo ya Halmashauri.

" ujenzi" ni pamoja na ukarabati wa majengo.

Mpango wa ujenzi

4. (1) Kwa madhumuni ya kudhibiti ujenzi holela, Halmashauri itaandaa mpango wa ujenzi.

(2) Mpango wa ujenzi utakaoandaliwa kwa mujibu wa kifungu kidogo cha (1) utaainisha aina ya majengo yanayopaswa kujengwa katika kila eneo la Halmashauri.

(3) Mtu yeyote anayetaka kujenga jengo jipya atatakiwa kufuata mpango wa ujenzi ulioandaliwa kwa mujibu wa kifungu kidogo cha (1)

Kibali cha ujenzi

5. (1) Bila kuathiri masharti ya sheria yoyote iliyotungwa na

Bunge, mtu yeyote hatoruhusiwa kujenga au kuweka jengo bila kupata kibali cha ujenzi kutoka Halmashauri.

(2) Kibali cha ujenzi kitatolewa kwa mwombaji baada ya kujaza fomu maalum itakayotolewa na Halmashauri na baada ya kulipa ada ya kibali kwa kiwango kilichoainishwa katika Jedwali la Kwanza la Sheria Ndogo hii.

(3) Nakala ya kibali cha ujenzi itabaki katika eneo la ujenzi kwa ajili ya ukaguzi.

Muda wa kutoa kibali

6. (1) Halmashauri itakuwa na wajibu wa kutoa kibali cha ujenzi chini ya Sheria Ndogo hii ndani ya muda wa siku thelathini tangu siku ya kupokelewa kwa maombi ya kibali cha ujenzi.

(2) Endapo Halmashauri itashindwa kutoa kibali cha ujenzi ndani ya muda ulioainishwa katika kifungu kidogo cha (1) itachukuliwa kuwa Halmashauri imeridhia kufanyika kwa ujenzi ulioombewa kibali na mwombaji atakuwa na haki ya kuanza ujenzi.

Notisi ya ubomoaji

7. (1) Halmashauri itakuwa na uwezo wa kumtaka mtu yeyote ambaye ameanzisha ujenzi wa jengo au kuweka jengo katika eneo la Halmashauri bila ya kuwa na kibali kilichotolewa kwa mujibu wa kifungu cha 6 kubomoa au kuondoa jengo husika.

(2) Notisi itakayotolewa kwa madhumuni ya kifungu kidogo cha (1) itamtaka mtu aliyepewa notisi hiyo kubomoa au kuondoa jengo ndani ya muda wa siku kumi na nne tangu tarehe ya kupokelewa kwa Notisi.

(3) Baada ya kumalizika kwa muda uliotolewa katika Notisi na endapo hakutakuwa na utekelezaji wa Notisi hiyo, Halmashauri itabomoa au kuondoa jengo na mtu aliyepewa Notisi atawajibika kulipa gharama zilizotumika kubomoa au kuhamisha jengo.

Makosa

8. (1) Itakuwa ni kosa kwa mtu yeyote kutenda mojawapo ya yafuatayo;-

(a) kujenga au kuanzisha shughuli za ujenzi pasipo kuzingatia masharti ya mpango wa ujenzi kwa mujibu wa kifungu cha 4 ch Sheria Ndogo hii.

(b) kujenga au kuweka jengo bila kuwa na kibali cha ujenzi kilichotolewa kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii;

(c) kujenga au kuweka jengo kinyume na masharti

ya kibali cha ujenzi kilichotolewa na Halmashauri; au

(d) kutobomoa au kuondoa jengo baada ya kupata Notisi ya Halmashauri iliyotolewa chini ya Sheria Ndogo hii.

(2) Mtu yeyote atakayetiwa hatiani kwa kosa lolote chini ya kifungu kidogo cha (1) atahukumiwa adhabu ya faini ya shillingi laki tatu au kifungo cha miezi sita jela au vyote kwa pamoja.

Kufifilisha kosa.

9. Bila kujali masharti ya kifungu kidogo cha (2) cha kifungu cha 8, Mkurugenzi anaweza kumtoza mtu yeyote kiasi cha shillingi laki moja iwapo mtu huyo atakiri kosa kwa kujaza fomu iliyoainishwa katika Jedwali la Pili la Sheria Ndogo hii na kukubali kutekeleza wajibu wake chini ya Sheria Ndogo hii.

JEDWALI LA KWANZA

*Limetungwa chini ya Kifungu cha 5(2)*

Sehemu ya kwanza

ADA YA UHAKIKI WA MAOMBI YA VIBALI VYA UJENZI

| NA. | AINA YA UENDELEZAJI | KIWANGO KILICHOPENDEKEZWA - (TShs.) |
|---|---|---|
| 1 | Majengo ya makazi | |
| | Jengo la kawaida | 50,000/= |
| | Jengo la ghorofa moja | 100,000/= |
| | Jengo la zaidi ghorofa moja | 200,000/= |
| | | |
| 2 | Majengo biashara | |
| | Jengo la kawaida | 60,000/= |
| | Jengo la ghorofa moja | 300,000/= |
| | Jengo la ghorofa mbili | 500,000/= |
| | Jengo la zaidi ghorofa mbili | 1,000,000/= |
| | | |
| 3 | Majengo ya viwanda/maghala | |
| | Jengo la kiwanda cha kawaida/ghala | 1,000,000/= |
| | Jengo la kiwanda cha kati/ghala | 1,500,000/= |
| | Jengo la kiwanda kikubwa/ghala | 2,000,000/= |
| | | |
| 4 | Vituo vya Mafuta | |
| | Kituo cha kuuza mafuta tu (filling station) | 500,000/= |
| | Kituo cha kuuza mafuta na kutoa huduma zingine (service station) | 1,000,000/= |
| | | |
| 5 | Nyumba za kupangisha (Housing Estate) | |
| | Nyumba ya kawaida | 60,000/= |
| | Nyumba ghorofa moja | 300,000/= |
| | Nyumba ya ghorofa mbili | 500,000/= |
| | Nyumba ya zaidi ya ghofa mbili | 1,000,000/= |
| 6 | Kuendeleza eneo bila kibali | 2% ya thamani ya jengo lililojengwa |

Sehemu ya pili

ADA ZA VIBALI VYA UJEZI MAENEO YALIYOPIMWA NA YASIYOPIMWA

| NA. | UKUBWA WA ENEO ($M^2$) | MAJENGO YA MAKAZI YA KAWAIDA | MAJENGO YA BIASHARA | MAJENGO YA VIWANDA/ MAGHALA | MAJENGO YA GHOROFA | MAJENGO YA UMMA |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | 0 - $50M^2$ | 50,000/= | 100,000/= | 150,000/= | 100,000/= | 40,000/= |
| 2 | 51 - 100 | 100,000/= | 200,000/= | 250,000/= | 200,000/= | 80,000/= |
| 3 | 101 - 150 | 150,000/= | 300,000/= | 350,000/= | 300,000/= | 120,000/= |
| 4 | 151 - 200 | 200,000/= | 400,000/= | 450,000/= | 400,00/= | 160,000/= |
| 5 | 201 - 300 | 250,000/= | 500,000/= | 550,000/= | 500,000/= | 200,000/= |
| 6 | 301 - 400 | 300,000/= | 600,000/= | 650,000/= | 600,000/= | 240,000/= |
| 7 | 401 - 500 | 350,000/= | 700,000/= | 750,000/= | 700,000/= | 280,000/= |
| 8 | 501 - 600 | 400,000/= | 800,000/= | 850,000/= | 800,000/= | 320,000/= |
| 9 | 601 - 700 | 450,000/= | 900,000/= | 950,000/= | 900,000/= | 360,000/= |
| 10 | 701 - 800 | 500,000/= | 1,000,000/= | 1,050,000/= | 1,000,000/= | 400,000/= |
| 11 | 801 - 950 | 700,000/= | 1,500,000/= | 1,550,000/= | 1,500,000/= | 500,000/= |
| 12 | Ongezeko kwa kila mita za mraba 100 | 50,000/= | 100,000/= | 150,000/= | 100,000/= | 40,000/= |
| 13 | UZIO kila Mzunguko wa mita moja | 500/= | 1,000/= | 1,050/= | 1,000/= | 500/= |

ADA YA VIBALI VYA UJENZI KWA HUDUMA NYINGINE

| | | MAKAZI | MAJENGO YA BIASHARA | MAJENGO YA VIWANDA/MAGHALA | MAJENGO YA UMMA |
|---|---|---|---|---|---|
| 14 | Kituo cha kuuza mafuta tu (filling station) kwa mita za mraba | - | 1000/= | 1050/= | 400/= |
| 15 | Kituo cha kuuza mafuta na kutoa huduma zingine (service station) kwa mita za mraba | - | 2000/= | 2050/= | 500/= |
| 16 | Eneo la maegesho ya magari kwa mita za | - | 1000/= | 1050 | 300/= |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | mraba | | | | |
| 17 | Eneo la kupunzika /burudani kwa mita ya mraba ya eneo lililoainishwa | - | 1000/= | 1050/= | - |
| 18 | Kiwanja cha michezo kwa mita za mraba | - | 1000/= | 1050/= | 200/= |
| 19 | Minara ya mawasiliano – kila mnara | - | 1,000,000/= | - | 500,000/= |
| 20 | Mabwawa ya kuogelea (swimming pools) kwa mita za mraba | 3,000/= | 4,000/= | 5,000/= | 2,500/= |
| 21 | Mabwawa ya kufuga samaki kwa mita za mraba | 2,500/= | 3,000/= | 4,000/= | 2,000/= |
| 22 | Matamki ya mafuta /Gesi (kwa mita za ujazo ) | | | | |
| | 0-1000 $m^3$ | | 2,500,000/= | | |
| | 1001- 2500 $m^3$ | | 4,000,000/= | | |
| | 25001-4000 $m^3$ | | 5,500,000/= | | |
| | 4001-6000 $m^3$ | | 7,000,000/= | | |
| | Ongezeko la kila mita za ujazo 500 | | 350,000/= | | |
| 23 | Minara ya matenki ya maji kwa mita ya mraba | 5,000/= | 8,000/= | 9,000/= | 4,000/= |
| 24 | Matenki ya maji kwa kila mita 1000 za ujazo | 2,000/= | 3,000/= | 4,000/= | 1,500/= |
| 25 | Ukarabati mdogo(Renovation) | 50,000/= | 100,000/= | | 40,000/= |
| 26 | Ukarabati mkubwa | 50% ya ada zilizoorodheshwa katika jedwali hili | 75% ya ada zilizoorodheshwa katika jedwali hili | 80% ya ada zilizoorodheshwa katika jedwali hili | 50% ya ada zilizoorodheshwa katika jedwali hili |
| 27 | Nyumba za kupangisha (Housing Estate) | | | | |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | Nyumba ya kawaida | 60,000/= | | | |
| | Nyumba ghorofa moja | 300,000/= | | | |
| | Nyumba ya ghorofa mbili | 500,000/= | | | |
| | Nyumba ya zaidi ya ghofa mbili | 1,000,000/= | | | |

JEDWALI LA PILI

*Limetungwa chini ya Kifungui cha 9*

HATI YA KUKIRI NA KUFIFILISHA KOSA

Mimi ......................................................................................................

Wa S.L.P.......................nakiri kwa hiari yangu mwenyewe mbele ya ........................................................ ambaye ni Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Mkuranga. Kwamba, tarehe................ ya mwezi........................mwaka........................... nilitenda kosa la kukiuka masharti ya Kifungu cha ..............................cha Sheria Ndogo ya Uthibiti wa Ujenzi Holela ya Halmashauri ya Wilaya ya Mkuranga za mwaka 2021.

Kwa hiyo, kwa hiyari yangu mwenyewe na bila kushawishiwa na mtu yeyote, nakubali kulipa kiasi cha shillingi laki moja kwa kutimiza wajibu chini ya Sheria Ndogo hiyo badala ya kushtakiwa Mahakamani.

Nathibitisha kwamba maelezo hapo juu ni ya kweli na nimeyatoa kwa hiari yangu kwa kadri ya ufahamu wangu

Jina.................................saini.............................tarehe.................

Jina la Mkurugenzi wa Halmashauri................................................

Saini...........................................Terehe.................................

Muhuri wa Halmashauri ya Wilaya ya Mkuranga umebandikwa kwenye Sheria Ndogo hizi kufuatia Azimio lililopitishwa kwenye Mkutano wa Baraza la Madiwani uliofanyika mnamo tarehe 28 mwezi Januari 2021 mbele ya:-

ENG, MSHAMU A. MUNDE,
*Mkurugenzi Mtendaji*
*Halmashauri ya Wilaya ya Mkuranga*

MHE, MOHAMED S. MWERA
*Mwenyekiti*
*Halmashauri ya Wilaya ya Mkuranga*

NAKUBALI

Dodoma

UMMY A. MWALIMU (MB)
*Waziri wa Nchi OR - Tamisemi*

TANGAZO LA SERIKALI Na..896 la Tarehe 22/11/2019

SHERIA YA FEDHA YA SERIKALI ZA MITAA

(SURA 290)

---

# SHERIA NDOGO

---

*(Imetungwa chini ya Kifungu cha 7(1) na 16 (1))*

---

SHERIA NDOGO YA ADA NA USHURU WA MADINI YA UJENZI YA HALMASHAURI YA WILAYA YA MKURANGA YA MWAKA 2019

Jina

1. Sheria Ndogo hii itaitwa Sheria Ndogo ya Ada na Ushuru wa Madini ya Ujenzi ya Halmashauri ya Wilaya ya Mkuranga ya Mwaka 2019.

Tafsiri

2. Katika Sheria Ndogo hii isipokuwa itakapoelezwa vinginevyo;

"ada" maana yake ni malipo yatakayolipwa na mtu yeyote kwa Halmashauri kwa ajili ya kupata kibali kinachotolewa na Halmashauri kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii;

"Halmashauri" maana yake ni Halmashauri ya Wilaya ya Mkuranga;

"kibali" maana yake ni idhini au ruhusa ya maandishi inayotolewa kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii;

"madini ya ujenzi" maana yake ni tarazo, moramu, udongo, kifusi, kokoto, mawe, mchanga, chokaa na madini mengine yanyotumika katika ujenzi;

"Mkurugenzi" maana yake ni Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Mkuranga na ni pamoja na Afisa yeyote atakayeteuliwa kutekeleza majukumu kwa niaba ya Mkurugenzi;

"ushuru" maana yake ni tozo inayotozwa na Halmashauri kwa shughuli zinazohusu ununuzi wa

madini ya ujenzi katika eneo la Halmashauri;

"Wakala" maana yake mtu, taasisi, kikundi cha watu, kampuni au asasi iliyoteuliwa na Halmashauri kukusanya ushuru wa madini ya ujenzi kwa niaba yake.

Maombi ya kibali

3.- (1) Mtu, taasisi au kampuni inayokusudia kuanzisha machimbo ya madini ya ujenzi katika eneo la Halmashauri itatakiwa kuwasilisha kwa Mkurugenzi maombi ya kibali cha uchimbaji wa madini ya ujenzi kupitia fomu maalum itakayotolewa na Halmashauri.

(2) Maombi ya kibali yatatakiwa kuambatishwa na taarifa zifuatazo:

(a) leseni ya uchimbaji wa madini iliyotolewa na mamlaka husika

(b) aina ya madini yanayokusudiwa kuchimbwa;

(c) umiliki pamoja na ukubwa wa eneo linalokusudiwa kuchimbwa madini ya ujenzi;

(d) mpango wa utunzaji wa mazingira katika eneo la machimbo; na

(e) muhtasari wa kijiji ambacho uchimbaji wa madini ya ujenzi utafanyika ukuonyesha kukubaliana na uchimbaji huo.

(2) Mkurugenzi, ndani ya muda wa siku saba tangu kupokea maombi, atatakiwa kukagua eneo ambalo uchimbaji wa madini ya ujenzi unakusudiwa kufanyika ili kujiridhisha iwapo eneo hilo linafaa kwa shughuli za uchimbaji wa madini ya ujenzi.

(3) Mkurugenzi, ndani ya muda wa siku saba tangu kukamilika kwa ukaguzi wa eneo linaloombewa kibali atatakiwa kukubali au kukataa maombi hayo na endapo atakataa atatakiwa kutoa sababu za kukataa maombi hayo.

Wajibu wa mpewa kibali

4. Mtu, taasisi au kampuni iliyopewa kibali cha uchimbaji wa madini ya ujenzi itatakiwa:

(a) kulipa ada ya kibali iliyoainishwa katika Jedwali la Kwanza la Sheria Ndogo hii ambayo italipwa kila mwaka ambao shughuli ya uchimbaji wa madini ya ujenzi itakuwa ikifanyika;

(b) kuzingatia masharti ya Sheria Ndogo hii na masharti ya kibali cha uchimbaji wa madini ya ujenzi; na

(c) kulipa ushuru na tozo mbalimbali zitakazotozwa na Halmashauri kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii au Sheria Ndogo nyingine iliyotungwa na Halmashauri.

Muda wa uchimbaji na usafirishaji

5.- (1) Shughuli za uchimbaji, uuzaji na ununuzi wa madini ya ujenzi katika eneo la Halmashauri zitafanyika kuanzia saa kumi na mbili asubuhi hadi saa kumi na mbili jioni ya kila siku.

(2) Bila kujali masharti ya kifungu kidogo cha (1), Mkurugenzi anaweza kutoa kibali maalum kuruhusu shughuli za uchimbaji, uuzaji na ununuzi wa madini ya ujenzi kufanyika nje ya muda ulioainishwa katika kifungu kidogo cha (1).

(3) Kila mmiliki wa gari linalosafirisha madini ya ujenzi atatakiwa kuhakikisha kuwa gari hilo limefumikwa wakati wote wa usafirishaji wa madini ya ujenzi.

Ushuru wa madini ya ujenzi

6.- Kutakuwa na ushuru wa madini ya ujenzi ambao utalipwa na mnunuzi au msafirishaji wa madini ya ujenzi kwa viwango vilivyoainishwa katika Jedwali la Kwanza la Sheria Ndogo hii.

Vituo vya ukaguzi

7.- (1) Kutakuwa na vituo vya ukaguzi wa malipo ya ushuru wa madini ya ujenzi katika njia zinazoingia au kutoka katika maeneo ya machimbo ya madini ya ujenzi.

(2) Kila dereva wa gari au chombo chochote cha usafiri kilichobeba madini ya ujenzi atatakiwa kusimama katika kituo cha ukaguzi wa malipo ya ushuru wa madini ya ujenzi na kuonyesha stakabadhi ya kielektroniki kuthibitisha kulipwa kwa ushuru wa madini ya ujenzi yaliyo katika gari au chombo cha usafiri anachoendesha.

Matumizi ya stakabadhi ya kielektroniki

8. Halmashauri au Wakala atatakiwa kutoza ada au ushuru kwa kadri itakavyokuwa kwa kutumia mashine za kielektroniki.

Kufutwa au kusimamishwa kwa kibali

9.- (1) Mkurugenzi anaweza kufuta au kusimamisha kibali cha uchimbaji wa madini ya ujenzi endapo atajiridhisha kuwa kuna ukiukwaji wa masharti ya Sheria Ndogo hii au masharti ya kibali cha uchimbaji wa madini ya ujenzi.

(2) Kwa kuzingatia masharti ya kifungu kidogo cha (1), Mkurugenzi kabla ya kufuta au kusimamisha kibali atatakiwa kutoa notisi ya siku saba kwa mtu, taasisi au kampuni iliyopewa kibali ya kusudio la kufuta au kusimamisha kibali.

(3) Notisi itakayotolewa kwa mujibu wa kifungu kidogo cha (2) itaainisha sababu za kufuta au kusimamisha kibali husika.

(4) Endapo kibali kitafutwa au kusimamishwa, mtu, taasisi au kampuni iliyopewa kibali cha uchimbaji wa madini ya ujenzi itakoma kuchimba madini hayo.

Wakala

10. Halmashauri inaweza kuteua mtu, kikundi cha watu, taasisi au kampuni kukusanya ushuru kwa niaba ya Halmashauri.

Makosa na adhabu

11. Mtu yeyote ambaye:

(a) ataanzisha machimbo ya madini ya ujenzi bila kuwa na kibali kilichotolewa chini ya Sheria Ndogo hii;
(b) atasafirisha madini ya ujenzi bila kulipa ushuru;
(c) atachimba madini ya ujenzi kabla au baada ya muda ulioruhusiwa kuchimba;
(d) atasafirisha madini ya ujenzi katika gari ambalo halijafunikwa; au
(e) atamshawishi mtu au kundi la watu kutolipa

ushuru,

atakuwa ametenda kosa na akipatikana na hatia atatozwa faini isiyopungua shilingi laki Mbili na isiyozidi shilingi milioni moja au kifungo kisichopungua miezi kumi na mbili na kizichozidi miezi ishirini na nne au adhabu zote mbili kwa pamoja yaani faini na kifungo

Kufifilisha kosa

12. Mkurugenzi anaweza kufifilisha kosa kwa kumtoza mtu yoyote aliyetenda kosa kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii kiasi cha shilingi laki mbili iwapo mkosaji atakiri kosa kwa hiari na kuwa tayari kujaza fomu maalum iliyoainishwa katika Jedwali la Pili la Sheria Ndogo hii na kuwa tayari kutimiza wajibu wake kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii.

## JEDWALI LA KWANZA

*(Limetengenezwa chini ya Kifungu cha 4(a) na 6)*

A: ADA YA KIBALI CHA UCHIMBAJI WA MADINI YA UJENZI

| NA | AINA YA MADINI | KIWANGO (TSH.) |
|---|---|---|
| 1. | Madini yote ya ujenzi | 1,000,000/= kwa kila kibali |

B: USHURU WA MADINI YA UJENZI

| NA | AINA YA MADINI | KIWANGO (TSH.) |
|---|---|---|
| 1. | Tarazo | 5,000/= kwa tani |
| 2. | Mawe | 5,000/= Kwa tani |
| 3. | Moramu | 4,000/= kwa tani |
| 4. | Kokoto | 6,000/= kwa tani |
| 5. | Udongo | 4,000/= kwa tani |
| 6. | Kifusi | 4,000/= kwa tani |
| 7. | Mchanga | 6,000/= kwa tani |
| 8. | Madini mengine yanayotumika katika ujenzi | 6,000/= kwa tani |

JEDWALI LA PILI

*(Limetengenezwa chini ya Kifungu cha 12)*

HATI YA KUFIFILISHA KOSA

Mimi.........................................nakiri kwa hiari yangu mwenyewe mbele ya................................................ambaye ni Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Mkuranga kwamba Tarehe......ya Mwezi................Mwaka ............nilitenda kosa la kukiuka masharti ya kifungu cha ..........................cha Sheria Ndogo ya Ada na Ushuru wa Madini ya Ujenzi ya Halmashauri ya Wilaya Mkuranga ya Mwaka 2019.

Kwa mamlaka aliyopewa Mkurugenzi wa Halmashauri niko tayari kulipa kiasi cha shilingi laki mbili na kutimiza wajibu wangu kwa mujibu wa Sheria Ndogo hiyo badala ya kushtakiwa Mahakamani.

NATHIBITISHA KWAMBA MAELEZO HAPO JUU NI YA KWELI NA NIMEYATOA KWA HIARI YANGU KADRI YA UFAHAMU WANGU

Leo Tarehe.....................ya

Mwezi....................Mwaka..........................

Jina.......................................

Saini.......................................

Mbele ya:

Jina...........................................

Cheo...........................................

Saini...........................................

TANGAZO LA SERIKALI NA. 896 *(linaendelea)*

Mhuri wa Halmashauri ya Wilaya ya Mkuranga ulibandikwa kwenye Sheria Ndogo hizi kwa kufuatia Azimio lililopitishwa kwenye mkutano wa Baraza la Madiwani uliofanyika mnamo tarehe 29 mwezi 05 mwaka 2018 mbele ya :-

ENG. MSHAMU A. MUNDE
*Mkurugenzi Halmashauri ya Wilaya ya Mkuranga*

L.S

MHE. JUMA A. ABEID
*Mwenyekiti Hlmashauri ya Wilaya ya Mkuranga*

KAKUBALI

Dodoma,
29 Oktoba, 2019

SELEMAN S JAFO (MB.)
*Waziri wan chi OR Tamisemi*

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA

*Supplement No. 47* *22th September,2019*

***SUBSIDIARY LEGISLATION***

*to the Gazette of the United Republic of Tanzania No.48. Vol.100 dated 22th September, 2019*
Printed by the Government Printer, Dodoma by Order of Government

TANGAZO LA SERIKALI NA-894 la tarehe 22/11/2019

SHERIA YA FEDHA YA SERIKALI ZA MITAA

(SURA 290)

# SHERIA NDOGO

*(Zimetengenezwa chini ya Kifungu cha 7(1) na 16 (1))*

## SHERIA NDOGO YA USHURU WA MAEGESHO NA STENDI YA HALMASHAURI YA WILAYA YA MKURANGA YA MWAKA 2019

Jina 1. Sheria Ndogo hii itajulikana kama Sheria Ndogo za Ushuru wa Maegesho na Stendi za Halmashauri ya Wilaya ya Mkuranga ya Mwaka 2019.

Matumizi 2. Sheria Ndogo hii itatumika katika eneo lote la Halmashauri ya Wilaya ya Mkuranga.

Tafsiri 3. Katika Sheria Ndogo hii isipokuwa pale itakavyoelezwa vinginevyo: -

"Afisa Mwidhiniwa" maana yake ni afisa yeyote wa Halmashauri anayesimamia utekelezaji wa Sheria Ndogo hii;

"chombo cha usafiri" maana yake ni chombo cha moto na ni

pamoja na gari, aina zote za pikipiki zikiwemo zenye magurudumu matatu, tela na mitambo yenye magurudumu au mnyororo;

"eneo la maegesho" maana yake ni lililotengwa na Halmashauri kwa ajili ya maegesho ya vyombo vya usafiri isipokuwa hifadhi ya barabara;

"Halmashauri" maana yake ni Halmashauri ya Wilaya ya Mkuranga;

"kuegesha" maana yake ni kusimamisha chombo cha usafiri katika eneo la maegesho kwa muda unaozidi dakika tano;

"mmiliki" maana yake ni mtu yeyote mwenye udhibiti wa chombo cha usafiri kilichoegeshwa kwenye eneo la maegesho;

"Mkurugenzi" maana yake ni Mkurugenzi wa Halmashauri na ni pamoja na afisa yeyote aliyeteuliwa kutekeleza majukumu ya Mkurugenzi;

"ushuru wa maegesho" maana yake ni tozo inayotozwa na Halmashauri kwa ajili ya maegesho ya vyombo vya usafiri;

"ushuru wa stendi" maana yake ni tozo inayotozwa na Halmashauri kwa mtu yeyote anayeingiza chombo cha usafiri katika eneo la stendi;

"Wakala" maana yake Wakala wa Halmashauri;

"yadi" maana yake ni eneo la Halmashauri lililotengwa kwa ajili ya kuhifadhi vyombo vya usafiri.

Wajibu wa kuanzisha maegesho

4.- (1) Halmashauri itakuwa na wajibu wa kutenga maeneo kwa ajili ya kuanzisha maegesho ya vyombo vya usafiri

(2) Katika kuteleza masharti ya kifungu kidogo cha (1), Halmashauri itakuwa na wajibu wa:-

(a) kuweka alama au maandishi ya kuzuia kuegesha vyombo vya usafiri au aina fulani ya vyombo vya usafiri kwenye maeneo ya maegesho;

(b) kuweka alama katika maeneo ya maegesho

kwa upana na urefu utakaokadiriwa kuegesha vyombo vya usafiri vilivyoidhinishwa kuegeshwa katika eneo husika; na

(c) kuweka matangazo yanayoainisha maeneo yanayoruhusiwa kuegesha au kulaza magari na maeneo yasiyoruhusiwa kuegesha au kulaza magari.

Ushuru wa maegesho

5.- (1) Halmashauri itatoza ushuru wa maegesho kwa chombo cha usafiri ambacho kitaegeshwa katika maeneo ya maegesho.

(2) Viwango vya ushuru wa maegesho vitatozwa na Halmashauri kwa kuzingatia uzito wa chombo cha usafiri na muda ambao chombo cha usafiri kitakuwa kimeegeshwa kama ilivyoanishwa katika Jedwali la Kwanza la Sheria Ndogo hii.

Msamaha wa kulipa ushuru maegesho

6.- (1) Vyombo vya usafiri ambavyo havitatozwa ushuru wa maegesho ni vifuatavyo:

(a) vyombo vya usafiri vinavyomilikiwa na Serikali vyenye namba rasmi za usajili zinazotumiwa na vyombo vya usafiri vya Serikali;

(b) vyombo vya usafiri vinavyomilikiwa na taasisi zenye hadhi ya kidiplomasia;

(c) vyombo vya usafiri vinavyoegeshwa katika maeneo ya maegesho yaliyo karibu na sehemu mahsusi za ibada wakati wa ibada;

(d) vyombo vya usafiri vinavyoegeshwa katika maeneo ya maegesho wakati wa shughuli maalum za kitaifa; na

(e) vyombo vya usafiri vinavyotumiwa na watu wenye ulemavu kwa matumizi binafsi.

TANGAZO LA SERIKALI NA. *894 (LINAENDELEA)*

(2) Bila kuathiri masharti kifungu kidogo cha (1), Halmashauri inaweza kutoa msamaha wa kulipa ushuru wa maegesho kupitia kibali maalum kitakachotolewa na Mkurugenzi.

Ushuru wa stendi

7.- (1) Halmashauri itatoza ushuru wa stendi kwa vyombo vya usafiri vinavyoingia katika eneo la stendi kwa namna na kiasi kilichoainishwa katika Jedwali la Pili la Sheria Ndogo hii.

(2) Ushuru wa stendi utatozwa kwa kila chombo cha usafiri kinapotoka nje ya eneo la stendi kwa ajili ya kuanza au kuendelea na safari.

Wajibu wa kutumia stendi

8.- (1) Kila mmiliki wa gari la abiria au gari la mizigo linalotoka au kwenda nje ya eneo la Halmashauri au ndani ya eneo la Halmashauri atatakiwa kuhakikisha kuwa gari lake linaingia katika eneo la stendi kwa ajili ya kuchukua au kushusha abiria au mizigo.

(2) Isipokuwa kwa kibali maalum cha Halmashauri, mabasi yote yanatakiwa kuanza safari zake katika maeneo ya stendi.

Ushuru wa kulaza vyombo vya usafiri

9. Halmashauri itatoza ushuru wa kulaza vyombo vya usafiri katika eneo la stendi, maegesho au yadi kwa na namna na viwango vilivyoainishwa katika Jedwali la Tatu la Sheria Ndogo hii.

Wajibu wa kulipa ushuru wa maegesho, stendi au yadi

10.- (1) Kila mmiliki wa chombo cha usafiri:

(a) atakayeegesha chombo chake katika eneo la maegesho;

(b) atakayeingiza chombo chake katika eneo la stendi au kulaza gari katika eneo la stendi au yadi,

atatakiwa kulipa ushuru wa maegesho, stendi au wa

kulaza gari kwa kadri itakavyokuwa kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii.

(2) Kila mmiliki atakayelipa ushuru wowote chini ya Sheria Ndogo hii atawajibika kuhakikisha anapewa stakabadhi ya kielektroniki mara tu anapolipa ushuru ikionesha thamani halisi ya fedha iliyolipwa.

(3) Mmiliki anayeegesha chombo cha usafiri katika eneo la maegesho au kuingiza chombo chake katika eneo la stendi au kulaza chombo chake katika eneo la stendi au yadi atakuwa na wajibu wa kuhakikisha usalama wa chombo na mali zilizomo ndani ya chombo chake.

(4) Halmashauri haitawajibika kwa namna yoyote kwa uharibifu au upotevu wa chombo kilichoegeshwa katika eneo la maegesho, stendi au yadi au mali zilizomo ndani ya chombo hicho.

Ada ya usajili

11.-(1) Mmiliki wa chombo cha usafiri kinachotumika kwa madhumuni ya kibiashara ndani ya eneo la Halmashauri atatakiwa kusajili chombo hicho kwa Halmashauri baada ya kulipa ada ya usajili iliyoainishwa katika Jedwali la Nne la Sheria Ndogo hii.

(2) Ada ya usajili wa chombo cha usafiri italipwa kila mwaka.

Matumizi ya Wakala

12. Halmashauri inaweza kuingia mkataba na kampuni kwa ajili ya kutoza ushuru chini ya Sheria Ndogo hii.

Matumizi ya mashine za kielektroniki

13.-(1) Halmashauri au Wakala utatoza ushuru ulioainishwa chini ya Sheria Ndogo hii kwa kutumia mashine za kielektroniki zitakazotoa stakabadhi yenye nembo, namba maalum za utambulisho wa mashine husika, namba ya chombo cha usafiri, tarehe, muda, kiasi na alama nyingine ambazo Halmashauri itaona zinafaa kuwemo.

(2) Mkusanya ushuru ulioainishwa chini ya Sheria Ndogo hii atatakiwa kuwa na kitambulisho au sare maalum yenye nembo ya Halmashauri au vyote kwa pamoja.

(3) Mkurugenzi au Afisa Mwidhiniwa atafanya ukaguzi wa

mara kwa mara ili kujiridhisha na matumizi sahihi ya mashine za kielektroniki na uzingatiaji wa uvaaji wa sare na vitambulisho.

Usimamizi wa Sheria Ndogo

14.-(1) Katika kusimamia utekelezaji wa Sheria Ndogo hii, Halmashauri au Wakala, kwa idhini ya Halmashauri unaweza: -

(a) kuzuia kuondolewa kwa chombo cha usafiri kutoka katika eneo la maegesho;

(b) kufunga chombo cha usafiri kwa vifaa maalum, kukinyanyua au kukivuta kwa lengo la kukipeleka sehemu ya kuhifadhiwa;

(c) kuondoa na kuweka chini ya uangalizi wake maliyoyote inayohamishika iliyowekwa kwenye eneo la maegesho bila ya kuwa na kibali cha maandishi cha Halmashauri baada ya kutoa notisi ya siku zisizozidi thelathini kwa mmiliki wa mali hiyo;

(d) kuondoa mali yoyote isiyohamishika iliyowekwa kwenye eneo la maegesho bila ya kuwa na kibali cha maandishi cha Halmashauri baada ya kutoa notisi ya siku thelathini kwa mmiliki wa mali hiyo;

(e) kuuza kwa njia ya mnada wa hadhara, baada ya kupata amri ya mahakama, mali yoyote iliyohifadhiwa na Halmashauri kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii kwa muda usiopungua miezi sita.

(2) Mtu yoyote hataruhusiwa kuchukuwa mali yake iliyohifadhiwa na Halmashauri hadi atakapolipa gharama zilizotumika katika kutekeleza masharti yakifungu kidogo cha (1).

Makosa na adhabu

15.- Mtu yeyote ambaye: -

(a) atafanya shughuli yoyote katika eneo la maegesho, stendi au yadi bila ya kuwa na kibali cha maandishi cha Halmashauri;

(b) ataweka vizuizi vya aina yoyote katika eneo la maegesho, stendi au yadi bila ya kuwa na kibali cha maandishi cha Halmashauri;

(c) ataegesha chombo cha usafiri katika eneo la maegesho, stendi au yadi nje ya mistari iliyochorwa kwa ajili ya kutenganisha sehemu za maegesho katika eneo la maegesho, stendi au yadi;

(d) ataegesha chombo cha usafiri katika eneo la maegesho, stendi au yadi kwa kutofuata mwelekeo wa mistari iliyochorwa;

(e) ataegesha chombo cha usafiri katika eneo la maegesho, stendi au yadi kwa namna ambayo inazuia chombo cha usafiri cha mmiliki mwingine;

(f) ataegesha chombo cha usafiri katika njia zinazotumika ndani ya eneo la maegesho, stendi au yadi;

(g) ataegesha chombo cha usafiri kwenye njia za kuingilia na kutokea katika maeneo ya maegesho, stendi au yadi;

(h) atakataa au kushindwa kulipa ushuru ulioainishwa chini ya Sheria Ndogo hii;

(i) atatelekeza chombo cha usafiri kwenye maeneo ya maegesho kwa zaidi ya muda wa kutoza ushuru wa maegesho chini ya Sheria Ndogo hii;

(j) atachafua maeneo ya maegesho;

(k) ataosha chombo cha usafiri katika eneo la maegesho;

(l) atafanya matengenezo ya chombo cha usafiri yasiyo ya dharura bila idhini ya Halmashauri au Wakala;

(k) ataharibu stakabadhi iliyotolewa na Halmashauri kabla ya kulipa ushuru wa maegesho;

(m) ataegesha chombo cha usafiri cha aina,

ukubwa au uzito usioruhusiwa katika eneo la maegesho;

(n) ataharibu vibao, samani au alama zinazotoa maelekezo katika maeneo ya maegesho, stendi au yadi;

(o) atajaribu au kufanya udanganyifu kwa nia ya kukwepa kulipa ushuru wa maegesho;

(p) ataegesha, bila sababu za msingi, chombo cha usafiri katika eneo ambalo si la maegesho;

(q) atachukua au kushusha abiria katika eneo ambalo si la stendi;

(r) basi lake litaanza safari nje ya eneo la stendi; au

(s) atashindwa kusajili chombo cha usafiri kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii,

atakuwa ametenda kosa na akipatikana na hatia atatozwa faini ya kiasi kisichopungua shilingi laki mbili na kisichozidi shilingi milioni moja au kifungo kisichopungua miezi kumi na mbili na kisichozidi miezi ishirini na nne au vyote kwa pamoja.

Kufifilisha a kosa

16. Mkurugenzi anaweza kufifilisha kosa lililotendwa chini ya Kifungu cha 15 kwa kutoza kiasi cha shilingi laki mbili kwa mtu yeyote ambaye atakiri kosa kwa kujaza fomu iliyoanishwa katika Jedwali la Tano la Sheria Ndogo hii.

Fidia

17. Bila kuathiri masharti ya Sheria Ndogo hii, mtu yeyote atayetiwa hatiani au kukiri kosa chini ya Kifungu cha 16 na ambaye amesababisha uharibifu katika eneo la maegesho, stendi au yadi atatakiwa kutengeneza eneo lililoharibika chini ya usimamizi wa Halmashauri.

JEDWALI LA KWANZA

*(Limetengenezwa chini ya Kifungu cha 5(2))*

USHURU WA MAEGESHO

| *Na.* | *Aina ya Gari* | *Kiasi cha ushuru kwa saa* | *Kiasi cha ushuru kwa siku* | *Kiasi cha ushuru kwa mwezi* | *Egesho lililotengwa kwa mwaka* |
|---|---|---|---|---|---|

*TANGAZO LA SERIKALI NA. 894 (LINAENDELEA)*

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| i. | Teksi | 200/= | 1,000/= | 20,000/= | 200,000/= |
| ii. | Gari dogo | 200/= | 1,000/= | 20,000/= | 200,000/= |
| iii. | Lori kuanzia chini ya tani 5 | 300/= | 2,000/= | 50,000/= | 500,000/= |
| iv. | Lori kuanzia tani 5 hadi tani 10 | 400/= | 4,000/= | 100,000/= | 1,000,000/= |
| v. | Lori zaidi ya tani 10 | 500/= | 5,000/= | 130,000/= | 1,300,000/= |
| vi. | Pick up | 200/= | 1,000/= | 20,000/= | 200,000/= |
| vii. | Aina nyingine za magari | 200/= | 1,000/= | 20,000/= | 200,000/= |
| viii. | Pikipiki ya matairi mawili | 100/= | 100/= | 3,000/= | 36,000/= |
| ix. | Pikipiki ya matairi matatu | 100/= | 100/= | 3,000/= | 36,000/= |

## JEDWALI LA PILI

*(Limetengenezwa chini ya Kifungu cha 7(1))*

USHURU WA MAGARI YANAYOINGIA STENDI

| *Na.* | *Aina ya Gari* | *Kiasi cha ushuru kwa safari moja(Tripu)* |
|---|---|---|
| i | Teksi | 500/= kwa tripu |
| ii | Bajaji | 300/= kwa tripu |
| iii | Pikipiki | 200/= kwa tripu |
| iv | Basi la abiria kuanzua 5-15 | 500/= kwa tripu |
| v | Basi la abiria chini ya 25 | 1,000/= kwa tripu |
| vi | Basi la abiria kuanzia 26-65 | 3,000/= kwa tripu |
| vii | Gari dogo la mizigo | 500/= kwa tripu |
| viii | Gari kubwa la mizigo | 2,000/= kwa tripu |

TANGAZO LA SERIKALI NA. 894 (LINAENDELEA)

| | | |
|---|---|---|
| ix | Magari mengineyo madogo | 500/= kwa tripu |
| x | Magari mengineyo makubwa | 2,000/= kwa tripu |
| xi | Magari mengine ambayo hayakutajwa | 2,000/= kwa tripu |

JEDWALI LA TATU

*(Limetengenezwa chini ya Kifungu cha 9)*

USHURU WA KULAZA VYOMBO VYA USAFIRI

| *Na.* | *Aina ya Gari* | *Kiasi cha ushuru kwa siku* |
|---|---|---|
| i. | Basi la abiria zaidi ya 40. | 10,000/= |
| ii. | Basi la abiria chini ya 40 | 5,000/= |
| iii. | Basi la abiria chini ya 20 | 2,000/= |
| iv. | Teksi | 1,500/= |
| v. | Gari dogo la kawaida | 1,000/= |
| vi. | Pick up au Station Wagon | 1,500/= |
| vii. | Guta | 200/= |
| viii. | Pikipiki ya matairi mawili | 400/= |
| ix. | Pikipiki ya matairi matatu | 500/= |
| x. | Gari la mizigo chini ya tani 5 | 3,000/= |
| xi. | Gari la mizigo kuanzia tani 5 hadi 10 | 5,000/= |
| xii. | Gari la mizigo zaidi ya tani 10 | 10,000/= |
| xiii. | Magari mengineyo madogo | 1,000/= |
| xiv. | Magari mengineyo makubwa | 2,000/= |
| xv. | Magari mengine ambayo hayakutajwa | 5,000/= |

JEDWALI LA NNE

*(Limetengenezwa chini ya kifungu cha 11)*

ADA YA USAJILI

| *Na.* | *Aina ya Gari* | *Kiasi cha Ada* |
|---|---|---|
| i. | Teksi | 7,500/= |
| ii. | Gari dogo la mizigo | 6,500/= |
| iii. | Lori chini ya tani 5 | 8,000/= |
| iv. | Lori tani 5 hadi tani 10 | 10,000/= |
| v. | Lori zaidi ya tani 10 | 15,000/= |
| vi. | Pick up | 5,000/= |
| vii. | Aina nyingine za magari | 10,000/= |
| viii. | Pikipiki ya matairi mawili | 5,000/= |

*Tangazo La Serikali Na. 894 (Linaendelea)*

| | | |
|---|---|---|
| ix. | Pikipiki ya matairi matatu (Bajaji) | 5,000/= |

JEDWALI LA TANO
*(Limetengenezwa chini ya kifungu cha 16)*

HATI YA KUFIFILISHA KOSA

Mimi........................ nakiri KWA HIARI YANGU MWENYEWE mbele ya ..........................ambaye ni Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Mkuranga kwamba Tarehe .........Mwezi.......... Mwaka.......... nilitenda kosa la kukiuka masharti ya kifungu cha.................. cha Sheria Ndogo ya Ushuru wa Maegesho na Stendi ya Halmashauri ya Wilaya ya Mkuranga ya Mwaka 2019.

Kwa mamlaka aliyopewa Mkurugenzi, niko tayari kulipa kiasi cha shilingi laki mbili pamoja na ushuru ninaodaiwa wa kiasi cha shilingi............... (Kama anayekiri kosa anadaiwa) na kulipa fidia ya kiasi cha shilingi..................... (kama anayekiri kosa amesababisha uharibifu) badala ya kushtakiwa Mahakamani.

NATHIBITISHA KWAMBA MAELEZO HAPO JUU NI KWELI NA NINAYATOA KWA HIARI YANGU KADRI YA UFAHAMU WANGU

Leo tarehe.................................... ya Mwezi.................Mwaka..............

Jina..............................................Saini.......................

Mbele ya:

Jina...........................................Cheo..................................

Saini.........................................Tarehe..................................

Mhuri wa Halmashauri ya Wilaya ya Mkuranga ulibandikwa kwenye Sheria Ndogo hizi kwa kufuatia Azimio lililopitishwa kwenye mkutano wa Baraza la Madiwani uliofanyika mnamo tarehe 29 mwezi 05 mwaka 2018 mbele ya :-

ENG. MSHAMU A. MUNDE

*Mkurugenzi Halmashauri ya*

*Wilaya ya Mkuranga*

**L.S**

MHE. JUMA A. ABEID

*Mwenyekiti Hlmashauri ya*

*Wilaya ya Mkurang*

KAKUBALI

Dodoma,

SELEMAN S JAFO (MB.)

29 Oktoba, 2019

*Waziri wan chi OR Tamisemi*

TANGAZO LA SERIKALI NA .895 La tarehe 22/11/2019

SHERIA YA FEDHA YA SERIKALI ZA MITAA

(SURA 290 )

# SHERIA NDOGO

*(Zimetungwa chini ya Kifungu cha 7(1) na 16 (1))*

SHERIA NDOGO YA USHURU WA MASOKO NA MAGULIO YA HALMASHAURI YA WILAYA YA MKURANGA YA MWAKA 2019

Jina

1. Sheria Ndogo hii itajulikana kama Sheria Ndogo ya Ushuru wa Masoko na Magulio ya Halmashauri ya Wilaya ya Mkuranga ya Mwaka 2019.

Matumizi

2. Sheria Ndogo hii itatumika katika eneo lote la Halmashauri ya Wilaya ya Mkuranga.

tafsiri

3. Katika Sheria Ndogo hii isipokuwa itakapoelezwa vinginevyo

"dalali" maana yake ni mtu yeyote anayeuza bidhaa za sokoni kwa njia ya mnada kwa niaba ya mwenye bidhaa kwa mujibu wa sheria na taratibu za soko;

"Halmashauri" maana yake ni Halmashauri ya Wilaya ya Mkuranga;

"kibali" maana yake ni idhini ya maandishi inayotolewa na Halmashauri kwa mujibu Sheria Ndogo hii;

"gazebo" maana yake ni kibanda chenye miguu ya chuma au plastiki au mbao ambacho juu yake kimefunikwa na paa la kitambaa au turubai au paa la aina yoyote;

"gulio" maana yake ni soko la wazi linalofanyika kwa wakati maalumu kwa kibali maalumu cha Halmashauri;

"kasha" maana yake ni kifaa maalumu cha kubebea au kuhifadhia bidhaa na mazao kama vile matenga, viroba,

magunia, karatasi ngumu, masanduku na mbao;

"soko" maana yake ni eneo maalumu la biashara lililotengwa na Halmashauri kwa matumizi ya kuuzia au kununulia bidhaa na ni pamoja na gulio;

"meza au kizimba" maana yake ni kitu au kifaa kinachotumika kuweka bidhaa kwa ajili ya kuuza sokoni au gulioni;

"mfanyabiashara" maana yake ni mtu yeyote anayeuza bidhaa sokoni au gulioni kwa jumla au rejareja;

"Mkuu wa Soko" maana yake ni mtu yeyote aliyeteuliwa au aliyeajiriwa na Halmashauri kusimamia shughuli zote katika soko;

"Mkurugenzi" maana yake ni Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Mkuranga;

"mnada" maana yake soko la wazi ambalo mali au vitu mbalimbali vinauzwa kwa ushindani wa bei kwa kauli na kwa kibali maalumu cha Halmashauri;

"wadau wa soko" maana yake ni mfanyabiashara binafsi, vikundi vilivyoandikishwa katika Kamati ya Wadau wa Soko au Gulio na kuwasilishwa kwa Mkuu wa Soko, au vyama vya ushirika vinavyofanya shughuli za biashara katika soko;

"Wakala" maana yake ni mtu, kikundi, taasisi au kampuni iliyopewa kazi ya kukusanya mapato ya Halmashauri katika chanzo au vyanzo vya mapato;

"ushuru" maana yake ni tozo inayolipwa baada au kabla ya kupata huduma katika soko au gulio;

"vikundi" maana yake ni vikundi vya ushirika vya wafanyabiashara au umoja wa vikundi vya wafanyabiashara vilivyosajiliwa au kuandikishwa na kuwasilishwa katika kamati ya Soko au Gulio na kwa Mkuu wa Soko na kutambuliwa na Halmashauri;

"zao" maana yake ni mavuno ya shambani au maliasili yanayoingizwa kwenye soko au ndani ya eneo la mamlaka ya Halmashauri.

Wajibu wa Halmashauri

4. Halmashauri itakuwa na wajibu wa:

(a) kuanzisha, kusimamia na kuendesha masoko kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii;

(b) kuendeleza masoko;

(c) kusimamia usafi na usalama wa masoko;

(d) kusimamia ufikishaji wa huduma za kijamii katika soko;

(e) kugawa na kupangisha soko kwa vyumba, meza au vizimba;

(f) kutenga maeneo kwa ajili ya magulio; na

(g) kusajili wafanyabiashara wote katika masoko yote ya Halmashauri.

Mkuu wa Soko

5.-(1) Kutakuwa na Mkuu wa Soko atakayeteuliwa na Halmashauri kwa ajili ya kusimamia shughuli za uendelezaji wa Masoko pamoja na:

(a) kukusanya ushuru na ada mbalimbali;

(b) kusimamia usajili wa wadau wa soko kwa kushirikiana na Kamati ya Wadau wa Soko;

(c) kuimarisha huduma za ulinzi, maji na umeme katika masoko;

(d) kusimamia usafi na uondoshaji wa taka katika soko;

(e) kuhakikisha kuwa bidhaa haziuzwi kwenye eneo ambalo haliruhusiwi kwa shughuli hiyo;

(f) kuzuia ujenzi holela katika soko; na

(g) kutekeleza majukumu mengine yeyote atakayoagizwa na Halmashauri.

(2) Bila kujali masharti ya kifungu kidogo cha (1), Halmashauri inaweza kuajiri Wakala ambaye atawajibika kusimamia uendeshaji wa soko kwa niaba ya Halmashauri.

(3) Wakala atakayeajiriwa chini ya kifungu kidogo cha (2) atasimamia shughuli za uendeshaji wa soko kwa kuzingatia masharti yaliyoainishwa katika kifungu kidogo cha (1) na masharti ya mkataba wa uwakala kati yake na Halmashauri.

Kamati ya Soko

6.- (1) Kutakuwa na Kamati ya Wadau wa Soko ambayo itaundwa na wadau wa soko kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii.

(2) Kila kikundi cha ushirika katika soko kitakuwa na mwakilishi mmoja katika Kamati ya Wadau wa Soko.

(3) Kamati ya Wadau wa Soko itatakiwa kuweka utaratibu maalum wa kuwapata viongozi wake, kuwaondoa madarakani na uendeshaji wa shughuli zake na kuuwasilisha kwa Hlamashauri.

(4) Vikao vya Kamati ya Wadau wa Soko vitafanyika mara moja kila mwezi.

(5) Mkuu wa Soko atakuwa Katibu katika vikao vyote vya Kamati ya Wadau wa Soko.

Majukumu ya Kamati

7. Kamati ya Wadau wa Soko itakuwa na majukumu yafuatayo:

(a) kuhakiki biashara zinazoendeshwa katika soko;

(b) kuboresha ustawi wa wadau wa soko;

(c) kuhakikisha uwepo wa nidhamu katika shughuli za soko;

(d) kuhakikisha wadau wote wa soko na gulio wanalipa ushuru na ada kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii;

(e) kukuza na kuendeleza mfumo wa biashara;

(f) kuhakikisha kila eneo la mdau na soko kwa ujumla linakuwa safi muda wote; na

(g) kutekeleza kazi nyingine watakazoelekezwa na Mkuu wa Soko kulingana na Sheria Ndogo hii.

Kamati Ndogo

8.- (1) Kamati ya Wadau wa Soko itaunda kamati ndogo zenye wajumbe wanne kutoka miongoni mwa wajumbe wa Kamati ya Wadau wa Soko ambazo ni:

(a) Kamati Ndogo ya Miundombinu na Usafi;

(b) Kamati Ndogo ya Utawala na Biashara; na

(c) Kamati Ndogo ya Ulinzi na Usalama.

(2) Bila kuathiri masharti ya kifungu kidogo cha (1), Kamati ya Wadau wa Soko inaweza kuunda kamati ndogo yoyote kwa kadri itakavyoona inafaa.

Usajili wa wadau

9.- (1) Mtu yeyote anayetaka kufanya biashara biashara katika eneo la soko atatakiwa kusajiliwa na Mkuu wa Soko akishirikiana na Kamati ya Wadau wa Soko kwa lengo la kumtambua na kumworodhesha katika rejesta ya wadau wa soko.

(2) Kwa kuzingatia masharti ya kifungu kidogo cha (1), kila mfanyabiashara atakayesajiliwa atapewa kibali cha kufanya biashara katika soko husika kutoka kwa Mkuu wa Soko kama kilivyoainishwa katika Jedwali la Kwanza la Sheria Ndogo hii.

(3) Kibali kitatatolewa kwa mfanyabiashara baada ya kulipa ada na kitadumu kwa muda wa mwaka mmoja tangu siku ya kutolewa na endapo atataka kuendelea na biashara katika soko atatakiwa kuomba kibali kingine kwa Mkuu wa Soko.

Utolewaji wa kibali kwa biashara ambazo hazikuwepo

10. Mtu au mfanyabiashara yeyote ambaye anataka kufanya biashara ambayo awali haikuwepo au haikuwa na eneo ndani ya soko ataomba kibali kwa Halmashauri na masharti ya kifungu cha 9 yatatumika.

Kufuta kibali

11.- (1) Mkuu wa Soko anaweza kufuta kibali kilichotolewa chini ya Sheria Ndogo hii, baada ya kutoa notisi ya siku thelathini, endapo mwenye kibali hicho:

(a) atakuwa na malimbikizo ya ada au ushuru;

(b) atakuwa amesimamisha shughuli zake kwa miezi mitatu bila taarifa;

(c) atakuwa na mwenendo unaokiuka masharti ya Sheria Ndogo hii;

(d) atawashawishi wafanyabiashara wengine kutofuata Sheria Ndogo hii au kusababisha uvunjaji wa amani; au

(e) atatumia chumba, kibanda, meza au kizimba alichopanga kinyume na madhumuni ya kufanyia biashara kama yalivyoainishwa kwenye mkataba wa upangishaji au maelekezo yatakayotolewa na Halmashauri.

(2) Mfanyabiashara ambaye hatoridhika na uamuzi wa kufutiwa kibali anaweza kiuwasilisha pingamizi lake kwa Mkurugenzi katika kipindi cha siku kumi na nne tangu tarehe ya kufutiwa kibali.

(3) Baada ya kupokea pingamizi, Mkurugenzi atatakiwa kutoa uamuzi wa pingamizi ndani ya siku saba tangu tarehe ya kupokea pingamizi husika.

Wajibu wa mfanyabiashara

**12.** Kila mfanyabiashara katika eneo la soko atakuwa na wajibu wa

(a) kusajiliwa na Mkuu wa Soko katika rejesta ya wadau wa soko;

(b) kulinda na kuhifadhi miundombinu ya soko;

(c) kufanya biashara katika maeneo yanayoruhusiwa;

(d) kufanya usafi katika eneo lake la biashara;

(e) kulipa ushuru na ada kwa wakati;

(f) kutobandika au kutobandua tangazo bila idhini ya Mkuu wa Soko;

(g) kutotumia lugha ya matusi, kuudhi au kashfa katika eneo la soko;

(h) kushiriki usafi wa jumla wa soko;

(i) kutoweka bendera ya chama chochote cha siasa ndani ya eneo la soko;

(j) kutofanya shughuli za kisiasa katika eneo la soko;

(k) kutotupa taka ovyo au kutiririsha maji machafu;

(l) kutowasha moto maeneo yasiyohusika ndani ya soko;

na

(m) kuheshimu masharti ya upangaji aliyopewa na Halmashauri na maelekezo atakayopewa na Halmashauri, Mkuu wa Soko na Kamati ya Wadau wa Soko.

Muda wa biashara

13.-(1) Soko litakuwa wazi siku zote kuanzia saa kumi na mbili asubuhi hadi saa kumi na mbili kamili jioni.

(2) Mkuu wa Soko, kwa kushauriana na Mkurugenzi, anaweza kufunga soko kwa ajili ya matengenezo au sababu nyingine yoyote ya dharura pale itakapoonekana inafaa.

(3) Isipokuwa kwa sababu nyingine za dharura, Mkuu wa Soko hatakuwa na mamlaka ya kufunga soko kwa sababu za matengenezo isipokuwa tu baada ya kutoa notisi ya siku saba kwa wadau wa soko kuhusu kusudio la kufunga soko kwa ajili ya matengenezo.

Ushuru wa soko au gulio

14.-(1) Halmashauri itatoza Ushuru wa Soko au Ushuru wa Gulio kutoka kwa kila mfanyabiashara aliyesajiliwa kufanya biashara katika eneo la soko au gulio kama ilivyoainishwa katika Jedwali la Pili la Sheria Ndogo hii.

(2) Bila kuathiri masharti ya kifungu kidogo cha (1), Halmashauri itatoza ushuru na ada ya kibali cha kuweka kioski, kibanda, kontena au genge la biashara lilio nje ya eneo la soko.

Ushuru wa kupakua na kubeba mizigo

15.-(1) Kutakuwa na ushuru utakaotozwa kwa kila gari litakaloingia ndani ya eneo la soko au barabara za soko kwa ajili ya kupakua au kubeba mizigo kama ilivyoanishwa katika Jedwali la Tatu la Sheria Ndogo hii.

(2) Magari yataruhusiwa kuingia katika eneo la soko kwa lengo la kupakua au kubeba mizigo kuanzia saa kumi na mbili asubuhi hadi saa kumi na mbili jioni.

Ada ya pango

16.-(1) Halmashauri itatoza ada ya pango la eneo la biashara katika soko ambayo italipwa na mfanyabiashara yeyote aliyesajiliwa kufanya biashara katika eneo la

soko.

(2) Halmashauri inaweza, kwa makubaliano maalum, kumruhusu mtu yeyote kujenga banda la biashara katika eneo la soko.

Kibali cha minada na magulio

17.-(1) Minada ya mazao, nguo na bidhaa nyingine itaruhusiwa kufanyika kwenye masoko kwa kibali maalum cha Halmashauri.

(2) Halmashauri inaweza kutoa kibali maalum cha kufanyika kwa magulio katika maeneo yatakayotengwa na Halmashauri.

Viwango vya ada na ushuru na muda wa kulipa

18.-(1) Viwango vya ada na ushuru vitakavyotozwa na Halmashauri kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii vitakuwa kama vilivyoainishwa katika Jedwali la Nne la Sheria Ndogo hii.

(2) Ada itakayotozwa chini ya Sheria Ndogo hii italipwa kabla ya huduma kutolewa.

(3) Ushuru unaotozwa chini ya Sheria Ndogo hii utalipwa kabla au wakati wa kupata huduma.

(4) Bila kuathiri masharti ya kifungu kidogo cha (3) cha Sheria Ndogo hii, Halamashauri inaweza kukubaliana na mlipa ushuru kuhusu utaratibu wa kulipa ushuru.

Usafi wa soko

19.-(1) Kila mfanyabiashara anayefanya biashara katika eneo la soko atawajibika kuweka eneo lake katika hali ya usafi wakati wote.

(2) Mkuu wa Soko kwa kushirikiana na Kamati ya Wadau wa Soko atasimamia usafi wa jumla wa soko siku ya Jumamosi ya mwisho wa mwezi.

(3) Kila mfanyabiashara atatakiwa kuzingatia kanuni za afya.

Huduma ndani ya soko

20. Kila mfanyabiashara katika soko atatakiwa kugharamia huduma ya ulinzi, usafi, maji na umeme kulingana na matumizi yake ya kila mwezi.

Uingizaji wa bidhaa

21.-(1) Bidhaa zote zitakazoingizwa katika soko zitatakiwa kuhifadhiwa kwenye makasha maalumu ya kusafirishia bidhaa.

(2) Ni marufuku kwa mkulima, mfanyabiashara, dalali au mtu mwingine yeyote kuingiza sokoni bidhaa zilizofungwa kwa majani au bidhaa zilizoharibika.

Mifugo kutoingizwa sokoni

22. Mtu yeyote hatoruhusiwa kuingiza mifugo katika eneo la soko isipokuwa mifugo ya jamii ya ndege na wanyama wadogo kama sungura watakaoletwa sokoni kwa ajili ya kuuzwa.

Tahadhari ya moto

23. Mtu yeyote hatoruhusiwa kufanya shughuli yoyote inayohusisha matumizi ya moto isipokuwa kwa idhini ya maandishi ya Halmashauri.

Makosa na adhabu

24. Mtu yeyote atakayekiuka au kwenda kinyume na kifungu chochote cha Sheria Ndogo hii atakuwa ametenda kosa na akipatikana na hatia atatozwa faini isiyopungua Shilingi laki mbili na isiyozidi Shilingi milioni moja au kifungo kisichopungua miezi kumi na mbili na kisichozidi miezi ishirini na nne au vyote faini na kifungo kwa pamoja.

Kufifilisha kosa

25. Bila kujali masharti ya kifungu cha 24, Mkurugenzi anaweza kumtoza mtu yeyote kiasi cha shilingi laki mbili endapo mtu huyo atakiri kosa kwa kujaza fomu iliyoainishwa katika Jedwali la Tano la Sheria Ndogo hii na kulipa kiasi hicho pamoja na ada au ushuru anaodaiwa iwapo kosa linahusisha kudaiwa ushuru au ada.

## JEDWALI LA KWANZA

*(Limetengenezwa chini ya kifungu cha 9 (2))*

### KIBALI CHA KUTUMIA SOKO/GULIO

1. Jina la Mwombaji ..........................................................
2. Anuani ya mwombaji ..........................................................
3. Kibali cha ..........................................................................
4. Eneo ambalo kibali hicho kitatumika ....................................
5. Muda wa Kibali ni kuanzia tarehe.....................hadi tarehe......
6. Masharti ya kutumia kibali hicho......................................
   a) ......................................................

b) ...............................................
c) ...............................................
d) ...............................................
e) ...............................................

7. Tarehe ya kikao kilichoidhinisha kibali....................................

Muhtasari Na...............

8. Imesajiliwa na:

Jina ...........................................

Saini.......................................... ......................................

Mkuu wa Soko Saini ya Mwombaji

Tarehe ...................................... Tarehe ..........................

Mhuri.......................................

JEDWALI LA PILI

*(Limetengenezwa chini ya kifungu cha 14)*

**USHURU WA MASOKO NA MAGULIO**

| Na. | Aina ya biashra | Ushuru |
|---|---|---|
| 1. | Biashara ya bidhaa mbalimbali za nafaka | 1,000/- kwa siku |
| 2. | Biashara ya samaki | 1,000/= kwa siku |
| 3. | Biashara ya chakula mama na baba lishe | 5,00/= kwa siku |
| 4. | Biashara ya vileo | 1,000/= kwa siku |
| 5. | Biashara ya kuchoma nyama | 2,000/= kwa siku |
| 6. | Biashara ya nguo za mitumba | 2,000/= kwa siku |
| 7. | Michezo mbalimbali katika soko | 2,000/= kwa siku |
| 8. | Biashara ya bidhaa za urembo | 1,000/= kwa siku |
| 9. | Biashara ya vyombo vya ndani | 1,000/= kwa siku |
| 10. | Biashara ya madukani | 1,000/= kwa siku |
| 11. | Biashara ya viatu vya mtumba | 1,000/= kwa siku |
| 12. | Biashara ya kuuza ndizi | 200/= kwa siku |
| 13. | Biashara ya kuuza bidhaa nyinginezo ambazo hazijatajwa | 200/= kwa siku |

JEDWALI LA TATU

*(Limetengenezwa chini ya kifungu cha 15 (1))*

| Na | Aina ya chanzo cha mapato | Ada ya siku |
|---|---|---|
| | Ushuru wa magari yanayoingia sokoni | |
| | 1.Tani 0 hadi 2.9 | 300/= kwa siku |
| | 2. Tani 3 hadi 3.9 | 500/= kwa siku |
| | 3.Tani 4 hadi 6.9 | 1,000/= kwa siku |
| | 4. Tani 7 hadi 40 na kuendelea | 3,000/= kwa siku |

JEDWALI LA NNE
*(Limetungwa chini ya kifungu cha 18 (1))*

ADA YA KUPANGISHA ENEO

| Na. | Aina ya chanzo cha mapato | Kiwango cha Ada |
|---|---|---|
| 1. | Vibanda | 40,000/= kwa mwezi |
| 2. | Vizimba | 10,000/=kwa mwezi |
| 3. | Eneo la machinjio ya kuku | 10,000/= kwa mwezi |
| 4. | Jengo la mama lishe | 10,000/= kwa mwezi |
| 5. | Jengo la kuhifadhia mizigo | 40,000/= kwa mwezi |
| 6. | Ofisi ndani ya soko | 40,000/= kwa mwezi |

JEDWALI LA TANO
*(Limetengenezwa chini ya kifungu cha 25)*

HATI YA KUKIRI NA KUFIFILISHA KOSA

Mimi ......................................... wa S.L.P. ............................................... nakiri kutenda kosa la ......................................................................... ikiwa ni kinyume na kifungu cha ................. cha Sheria ya Ndogo ya Ushuru wa Masoko na Magulio ya Halmashauri ya Wilaya ya Mkuraga ya Mwaka 2019.

Kwa hiari yangu mwenyewe pasipo kushawishiwa na mtu yeyote nakubali kulipa kiasi cha shilingi laki mbili na kutekeleza wajibu wangu chini ya Sheria Ndogo hiyo badala ya kushtakiwa Mahakamani iwapo Mkurugenzi atatekeleza madaraka aliyopewa chini ya kifungu cha.................................... cha Sheria Ndogo hiyo.

Saini: ........................................................

Tarehe ........................................................

Mbele yangu:-

Jina: ........................................................

Saini: ........................................................

Wadhifa: ........................................................

Tarehe ........................................................

Mhuri wa Halmashauri ya Wilaya ya Mkuranga ulibandikwa kwenye Sheria Ndogo hizi kwa kufuatia Azimio lililopitishwa kwenye mkutano wa Baraza la Madiwani uliofanyika mnamo tarehe 29 mwezi 05 mwaka 2018 mbele ya :-

ENG. MSHAMU A. MUNDE
*Mkurugenzi Halmashauri ya*
*Wilaya ya Mkuranga*

L.S

MHE. JUMA A. ABEID
*Mwenyekiti Hlmashauri ya*
*Wilaya ya Mkuranga*

KAKUBALI

Dodoma,
29 Oktoba, 2019

SELEMAN S JAFO (MB.)
*Waziri wan chi OR Tamisemi*

LEGAL UNIT COPY

ISSN 0856 – 034X

*Supplement No. 38* *1st October, 2010*

# *SUBSIDIARY LEGISLATION*

*to the Gazette of the United Republic of Tanzania No. 40 Vol. 91 dated 1st October, 2010*

Printed by the Government Printer Dar es Salaam, by Order of Government

TANGAZO LA SERIKALI NA. 365 la tarehe 1/10/2010

SHERIA YA FEDHA ZA SERIKALI ZA MITAA
(SURA YA 290)

## SHERIA NDOGO

*(Zimetungwa chini ya Vifungu vyo 7(1) na 16(1))*

SHERIA NDOGO ZA (KODI YA HUDUMA) ZA HALMASHAURI YA WILAYA YA MKURANGA, 2010

1. Sheria Ndogo hizi zitajulikana kama Sheria Ndogo za (Kodi ya Huduma) za Halmashauri ya Wilaya ya Mkuranga, 2010 na zitaanza kutumika mara baada ya kutangazwa kwenye gazeti la Serikali. Jina na mwanzo wa kutumika

2. Sheria Ndogo hizi zitatumika katika eneo lote la Halmashauri ya Wilaya ya Mkuranga. Matumizi

3. Katika Sheria Ndogo hizi, isipokuwa pale itakapoelezwa vinginevyo:- Tafsiri

"Afisa Aliyeidhinishwa" ina maana ya Afisa ye yote wa umma au mtu mwingine aliyeteuliwa na Halmashauri kusimamia utekelezaji wa Sheria Ndogo hizi;

"Halmashauri" maana yake ni Halmashauri ya Wilaya ya Mkuranga;

"Sheria" maana yake ni Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa Sura ya 290;

"Hesabu" ina maana ya jumla ya mauzo au manunuzi ikiwa ni pamoja na kodi na ada katika mwaka wa mapato;

"Hesabu za mwisho" ina maana ya hesabu za mwisho zinazowasilishwa na Taasisi yo yote ya kibiashara baada ya kipindi cha hesabu kwa mujibu wa aya ya 9 ya Sheria Ndogo hizi pamoja na nyaraka au maelezo yatakayotakiwa kutolewa kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi;

"Jumuisho" ina maana ya taarifa, nyaraka au hesabu au maelezo yo yote

yahusuyo kiasi na thamani ya kifedha ya bidhaa au huduma zilizozalishwa, zilizosambazwa, zilizotolewa na, au kuuzwa kibiashara na ikiwa ni pamoja na jumuisho la awali au la mwisho;

"Kipindi cha hesabu" ina maana ya muda ambao mfanyabiashara anatakiwa kuwasilisha hesabu za biashara zake;

"Mkurugenzi" maana yake ni Mkurugemzi mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Mkuranga pamoja na Afisa ye yote atakayeteuliwa kutekeleza majukumu ya Mkurugenzi;

"Mkusanya kodi" maana yake ni mtumishi au wakala aliyeteuliwa n Halmashauri kukusanya kodi kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi;

"Mwaka wa mapato" maana yake ni kipindi cha miezi kumi na mbili ya kalenda ya mwaka;

"Taasisi ya kibiashara" ina maana ya Taasisi iliyosajiliwa kwa mujibu wa Sheria ya Makampuni au Sheria ya majina ya kibiashara inayojihusisha na shughuli za kiuchumi za uzalishaji wa bidhaa au mazao ya kilimo, usambazaji wa bidhaa au utoaji wa huduma na, au biashara ikiwemo, usambazaji wa bidhaa au utoaji wa huduma na, au biashara ikiwemo uagizaji wa bidhaa kutoka nje ya nchi.

Utozaji wa kodi

4. Halmashauri itatoza na kukusanya kodi ya huduma kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi kutoka kwa kila taasisi ya kibiashara katika kila mwaka wa mapato ambayo ni sawa na asilimia sifuri nukta tatu (0.3) ya hesabu ya shughuli zote zikiwemo za uzalishaji wa bidhaa au huduma kutoka nje ya nchi zinazofanyika katika eneo la Halmashauri ukiondoa kodi ya ongezeko la thamani na kodi ya mlaji.

Uwasilishaji wa taarifa kuhusu shughuli za kibiashara

5. Mkuruge. [illegible] kwa aarifa ya maandishi, anaweza kumtaka mlipa ko[illegible] au mkusanya kodi ye , ote kuwasilisha hesabu zenye taarifa ka[illegible] z shughuli za kibia[illegible]ara z kionyesha thamani ya kiasi na thamani ya kifedha ya bidhaa au huduma zilizozalishwa, kutolewa, kusambazwa au kuuzwa kibiashara na taarifa ya fedha katika kipindi maalum kisichozidi siku thelathini tangu tarehe ya taarifa hiyo.

Uwasilishaji wa taarifa

6. Mkurugenzi anaweza kwa taarifa ya maandishi kumtaka mtu ye yote mwenye taarifa au maelezo kuhusu taasisi yo yote ya kibiashara inayopaswa kulipa Kodi kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi, kuwasilisha kwake taarifa au maelezo hayo katika kipindi kisichopungua siku thelathini tangu tarehe ya agizo hilo.

7. Mkurugenzi anaweza kumwagiza kwa maandishi Afisa Muidhiniwa kuingia kwenye jengo au eneo la Taasisi ya kibiashara au la mlipa au mkusanya Kodi ye yote kwania ya kufanya uchunguzi na tathmini ya kumbukumbu za biashara, vitabu vya hesabu, na taarifa nyinginezo kama atakavyoona inafaa kufanyiwa uchunguzi kwa ajili ya kupata na kujua kiwango sahihi cha kodi anachotakiwa kulipa mlipa kodi au mkusanya kodi hiyo. Uwezo wa kuingia kwenye jengo

8.-(1) Mkurugenzi anaweza, kwa taarifa ya maandishi, kumtaka mlipa kodi au mkusanya Kodi ye yote kuwasilisha kwake kumbukumbu za biashara na vitabu vya hesabu, kwa nia ya kupata taarifa kwa ajili ya kufanyiwa tathmini au kukusanya kodi ya huduma.

2. Kwa nia ya kupata taarifa kwa mujibu wa Sheria Ndogo ya 8(1) Mkurugenzi anaweza kumtaka mtu ye yote kufika mbele yake au kwa Afisa Muidhiniwa katika muda na mahali kadri atakavyoona inafaa.

9. Kila mlipa au mkusanya Kodi ya huduma atatakiwa kutoa na, au kuwasilisha hesabu za awali na kulipa Kodi anayotakiwa katika muda kama ifuatavyo:- Uwasilishaji

(a) kwa waagizaji bidhaa kutoka nje ya nchi watalipa kodi katika muda kama itakavyokuwa imeelekezwa na Kamishina wa Kodi ya forodha na Kodi ya mlaji;

(b) wazalishaji wa bidhaa za viwandani watalipa kodi kama itakavyokuwa imeelezwa na kamishna wa kodi ya Ongezeko la thamani (VAT isipokuwa haitakuwa zaidi ya muda wa kulipa Kodi ya mlaji au (VAT);

(c) watu wengine watalipa katika awamu nne (4) awamu ya kwanza ikianzia katika kipindi cha miezi mitatu baada ya kuanza kwa kipindi cha mahesabu.

10. Mkurugenzi anaweza kuteua kamishina wa Kodi ya forodha au Kodi ya mapato kutathmini na kukusanya Kodi ya huduma na kuwasilisha kwa Halmashauri kwa wakati kama ilivyoelekezwa kwenye Sheria Ndogo ya 9 kwa lengo la kufanya tathmini, kukusanya na kupata kodi pamoja na madeni yake. Uteuzi wa Mkusanya kodi

11.-(1) Kiwango cha Kodi kitakuwa ni asilimia 0.3% ya hesabu ya shughuli zote baada ya kuondoa Kodi ya ongezeko la thamani na kodi ya mlaji.

(2) Mkusanya Kodi au mlipa Kodi ye yote akishindwa kuwasilisha Kodi yake au ya mlipa Kodi, atachukuliwa kama hajalipa kodi na anastahili au kuwajibika kulipa kodi hiyo kama vile ndiye mlipa kodi ya Halmashauri, na njia zote za kukusanya madeni zitatumika dhidi yake kama vile ndiye mlipa kodi husika.

(3) Bila ya kuathiri masharti yaliyowekwa na Sheria Ndogo hizi Mkurugenzi anaweza kuteua wakala kukusanya kodi kwa niaba yake na wakala huyo atakuwa na jukumu la:-

(a) kuwasilisha majumuisho kwa Mkurugenzi au Afisa muidhiniwa;

(b) kuwasilisha kodi aliyokusanya katika kipindi maalum.

12.-(1) Kila mlipa kodi au mkusanya kodi atatakiwa kuwasilisha kwa Halmashauri hesabu za mwisho katika kipindi cha miezi minne tangu kumalizika kwa kipindi cha hesabu ya kodi anayostahili katika mkupuo mmoja.

(2) Mlipa kodi au mkusanya kodi anapowasilisha hesabu zake, Afisa muidhiniwa anaweza:-

(a) kupokea na kukubali hesabu hizo na kutathmini kodi katika msingi huo:

(b) kufanya tathmini kuhusu kiwango cha hesabu cha mlipa kodi huyo iwapo atakuwa na hisia za kimsingi za kuamini kuwa hesabu hizo siyo sahihi.

(3) Iwapo mlipa kodi hajawasilisha majumuisho ya hesabu zake kwa mwaka wo wote wa pato aidha ametakiwa kufanya hivyo na Mkurugenzi au Afisa muidhiniwa anafikiri kwamba mlipa kodi huyo ana wajibu wa kulipa kodi kwa mwaka huo, anaweza kwa kadri atakavyoona, kuamua kiwango cha hesabu za mlipa kodi huyo, isipokuwa tathmini hiyo haitaathiri wajibu wo wote wa mlipa kodi anayostahili kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi, kwa kushindwa kwake kuwasilisha hesabu hizo.

(4) kodi iliyotathminiwa kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi, italipwa katika siku thelathini tangu tarehe ya kufanya tathmini.

13.-(1) Mtu ye yote anayetakiwa kulipa kodi akishindwa kuwasilisha hesabu zake kama inavyotakiwa kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi katika kipindi kilichoongezwa atatozwa riba ya asilimia 1.5 kwa mwezi au shilingi elfu hamsini kutegemea kiwango kipi kitakuwa kikubwa.

(2) Iwapo mtu ye yote atasema uongo au ataficha baadhi ya hesabu zake kwa nia ya kupunguza kiwango cha kodi anachotakiwa kulipa, na inapobainika kuwa ufichaji au upunguzaji huo aliufanya kwa makusudi, mtu huyo atatozwa ushuru pamoja na nyongeza ya kodi ya asilimia hamsini (50%) ya tofauti kati ya kodi anayotakiwa kulipa na hesabu alizowasilisha pamoja na kiwango cha kodi halisi.

Jumla ya riba kutozwa kwenye kodi isiyolipwa

14.-(1) Kodi ambayo haijalipwa kwa wakati kama ilivyoelezwa kwenye Sheria Ndogo hizi, itatozwa riba ya jumla ya asilimia 15% kwa mwezi na itatakiwa kulipwa pamoja na kodi inayodaiwa.

(2) Riba itozwayo katika Sheria Ndogo hizi itachukuliwa kama kodi inayostahili kulipwa na njia zote za kukusanya kodi na madeni zitatumika kukusanya riba hiyo kama kodi inayolipwa na mlipa kodi huyo.

Kushindwa kutimiza maagizo

15. Mtu ye yote ambaye bila ya sababu za msingi:-

(a) atashindwa kuwasilisha hesabu sahihi na za kweli;

(b) atashindwa kuwasilisha nyaraka, maelezo au taarifa inayotakiwa kuwasilishwa kwa Halmashauri katika muda uliowekwa;

(c) atashindwa kutunza kumbukumbu, kitabu au hesabu;

(d) atashindwa kuonyesha kumbukumbu yo yote au nyaraka kwa ajili ya uchunguzi.

atakuwa ametenda kosa chini ya sheria Ndogo hizi.

Utoaji wa taarifa ya uongo

16. Mtu ye yote bila ya sababu za msingi:-

(a) akifanya hesabu za uongo kwa kupunguza au kutoa hesabu zisizokuwa sahihi;

(b) akitoa taarifa isiyokuwa sahihi kuhusu jambo lo lote linaloweza kuathiri jukumu lake au la mtu mwingine la kulipa kodi;

(c) akiandaa au kutengeneza au kusababisha kuandaliwa au kutengenezwa kwa vitabu vya uongo vya mahesabu au kumbukumbu;

(d) atamzuia au atajaribu kumzuia Afisa Muidhiniwa kutekeleza majukumu yake aliyopewa kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi, atakuwa ametenda kosa.

Adhabu

17.-(1) Mtu ye yote atakayevunja masharti ya Sheria Ndogo hizi atakuwa ametenda kosa na akitiwa hatiani atawajibika kulipa faini isiyozidi shilingi elfu hamsini (50,000/=) au atatumikia kifungo cha miezi isiyozidi kumi na mbili jela au adhabu zote mbili kwa pamoja yaani faini na kifungo.

(2) Pamoja na adhabu atakayopewa mkosaji katika Sheria Ndogo ya 17(1). mkosaji atawajibika kuilipa Halmashauri gharama iliyoingia kutokana na kuvunja masharti ya Sheria Ndogo hizi.

Kufifilisha kosa

18. Endapo mtu ametenda kosa na kukiri kwa maandishi kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi, Mkurugenzi anaweza kushughulikia kosa hilo na kuagiza kuwa mtu huyo alipe deni analodaiwa pamoja na adhabu ya kulipa faini isiyozidi shilingi mia tatu elfu.

Mhuri wa Halmashauri ya Wilaya ya Mkuranga ulibandikwa kwenye Sheria Ndogo hizi kwa kufuata azimio lililopitishwa na Mkutano wa Halmashauri ulioitishwa na kufanyika tarehe 29/04/2010 na ulibandikwa mbele ya :-

SIPORA J. LIANA,
*Mkurugenzi Mtendaji (W)*
*Halmashauri ya Wilaya ya Mkuranga*

L.S.

SHABAN S. MWELA,
*Mwenyekiti*
*Halmashauri ya Wilaya ya Mkuranga*

NAKUBALI,

Dodoma,
17 Julai, 2010

MHE. MIZENGO PETER PINDA (MB.),
*Waziri Mkuu*

TANGAZO LA SERIKALI NA . 967la Tarehe 6/12/2019

SHERIA YA FEDHA ZA SERIKALI ZA MITAA

(SURA 290)

# SHERIA NDOGO

*(Imetungwa chini ya kifungu cha 7(1)(z) na 16(1))*

SHERIA NDOGO YA USHURU WA HUDUMA (MAREKEBISHO) YA HALMASHAURI YA WILAYA WA MKURANGA YA MWAKA 2019

Jina

Tangazo la Serikali Na.365 la Mwaka 2010

1. Sheria Ndogo hii itajulikana kama Sheria Ndogo ya Ushuru wa Huduma (Marekebisho) ya Halmashauri ya Wilaya ya Mkuranga za Mwaka 2019 na itasomwa kwa pamoja na Sheria Ndogo za (Kodi za Huduma) za Halmashauri ya Wilaya ya Mkuranga za Mwaka 2010 ambayo katika Sheria Ndogo hii zitajulikana kama "Sheria Ndogo kuu".

Marekebisho ya kifungu cha 17 (1)

2. Sheria Ndogo kuu inafanyiwa marekebisho katika kifungu cha 17(1) kwa kufuta maneno "isiyozidi shilingi elfu hamsini (50,000/=)" na badala yake kuweka maneno "isiyopungua shilingi laki mbili na isiyozidi shilingi milioni moja"

Marekebisho ya kifungu cha 18

3. Sheria Ndogo kuu inafanyiwa marekebisho kwa kufuta kifungu cha 18 na badala yake kuweka kifungu kifuatacho:

Kufifilidha kosa

18 . Mkurugenzi anaweza kufifilisha kosa kwa kumtoza mtu yoyote aliyetenda kosa kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii kiasi cha shilingi laki mbili iwapo mkosaji atakiri kosa kwa hiari na kuwa tayari kujaza fomu maalum iliyoainishwa katika Jedwali la Sheria Ndogo hii na kuwa tayari kutimiza wajibu wake kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii.

Kuingiza Jedwali

4. Sheria Ndogo kuu inafanyiwa marekebisho kwa kuingiza Jedwali lifuatalo:

"JEDWALI

*(Limetengenezwa chini ya Kifungu cha 18)*

HATI YA KUFIFILISHA KOSA

Mimi…………………..…………..nakiri kwa hiari yangu mwenyewe mbele ya…………………ambaye ni Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Mkuranga kwamba Tarehe……ya Mwezi……………..Mwaka …………nilitenda kosa la kukiuka masharti ya kifungu cha …………………cha Sheria Ndogo za (Kodi ya Huduma) za Halmashauri ya Wilaya Mkuranga za Mwaka 2010.

Kwa mamlaka aliyopewa Mkurugenzi wa Halmashauri niko tayari kulipa kiasi cha shilingi laki mbili na kutimiza wajibu wangu kwa mujibu wa Sheria Ndogo hiyo badala ya kushtakiwa Mahakamani.

NATHIBITISHA KWAMBA MAELEZO HAPO JUU NI YA KWELI NA NIMEYATOA KWA HIARI YANGU KADRI YA UFAHAMU WANGU

Leo Tarehe…………………ya Mwezi…………..Mwaka………………………..

Jina………………………………..

Saini………………………………

Mbele ya:

Jina………………………………….

Cheo…………………………………

Saini…………………………………

Mhuri wa Halmashauri ya Wilaya ya Mkuranga ulibandikwa kwenye Sheria Ndogo hizi kwa kufuatia Azimio lililopitishwa kwenye mkutano wa Baraza la Madiwani uliofanyika mnamo tarehe 29 mwezi 05 mwaka 2018 mbele ya :-

ENG. MSHAMU A. MUNDE
*Mkurugenzi Halmashauri ya Wilaya ya Mkuranga*

L.S

MHE. JUMA A. ABEID
*Mwenyekiti Hlmashauri ya Wilaya ya Mkuranga*

KAKUBALI

Dodoma,
29 Oktoba, 2019

SELEMAN S JAFO (MB.)
*Waziri wan chi OR Tamisemi*

TANGAZO LA SERIKALI NA. 367 la tarehe 01/10/2010

SHERIA YA SERIKALI ZA MITAA (MAMLAKA ZA WILAYA)

(SURA YA 287)

# SHERIA NDOGO

*Zimetungwa chini ya Kifungu Na. 153*

SHERIA NDOGO ZA (HIFADHI YA MAZINGIRA) ZA HALMASHAURI YA WILAYA YA MKURANGA, 2010

## SEHEMU YA KWANZA
UTANGULIZI

1. Sheria Ndogo hizi zitaitwa Sheria Ndogo za (Hifadhi ya Mazingira) za Halmashauri ya Wilaya ya Mkuranga, 2010 na zitaanza kutumika baada ya kutangazwa kwenye Gazeti la Serikali. Jina na mwanzo wa kutumika

2. Sheria Ndogo hizi zitatumika katika maeneo yote ya Halmashauri ya Wilaya ya Mkuranga. Matumizi

3. Katika Sheria Ndogo hizi isipokuwa pale itakapoelezwa vinginevyo: Tafsiri

"Afisa mwidhinishwa" maana yake ni afisa maliasili, afisa kilimo na mifugo pamoja na afisa ye yote wa Halmashauri atakayeteuliwa kusimamia utekelezaji wa Sheria Ndogo hizi.

"Eneo la Hifadhi" ni maeneo ya milima, maeneo ya vyanzo vya maji, hifadhi ya misitu, miteremko na maeneo mengine ambayo yatatangazwa na Halmashauri kuwa ni maeneo ya hifadhi.

"Halmashauri" maana yake ni Halmashauri ya Wilaya ya Mkuranga.

"Hifadhi ya Mazingira" maana yake ni utunzaji endelevu wa ardhi, mimea, hewa, viumbe hai na visivyo hai na vyanzo vya maji vinavyozingatia masharti na maelekezo yatakayotolewa na afisa mwidhinishwa chini ya Sheria Ndogo hizi au Sheria nyingine ye yote.

"Kiwanda" maana yake ni jengo au kundi la majengo au eneo ambapo vitu vinatengenezwa.

"Kuvuna misitu" maana yake ni pamoja na kufyeka, kukata au kung'oa miti, visiki.

"Maeneo ya malisho" maana yake ni pamoja na sehemu zote ambazo zimetengwa na Halmashauri.

"Maji" kama ilivyotafsiriwa katika Sheria ya usimamizi Mazingira Na. 20 ya mwaka 2004 ni pamoja na maji ya kunywa, ya mito, vijito, maji yanayotiririka, yaliyohifadhiwa, yaliyo katika visima, mabwawa, mifereji, madimbwi, maziwa, maji yaliyoko chini ya ardhi, na maji yaliyoko katika mkondo.

"Maji taka" kama ilivyo katika Sheria ya usimamizi wa Mazingira Na. 20 ya mwaka 2004 ni pamoja na taka zinazotokana na kinyesi, mkojo na jasho, uchafu wa majimaji kutoka majumbani, taasisi, majengo ya biashara na viwandani.

"Mazao ya misitu" maana yake kama ilivyotafsiriwa katika Sheria ya Misitu Na. 14 ya mwaka 2002 chini ya kifungu Na. 2 ni kitu cho chote kinachopatikana au kuzalishwa kutokana na miti, mazao yanayoota au kupatikana msituni, ambayo ni pamoja na mianzi, magamba, mkaa, kuni, miti, fito, mbao, mbegu za miti, nta, asali, utaa, matunda, upapi, majani ya kulalia wanyama majani, mizizi, gundi, utomvu, maranda, matete, kamba, makuti (mawale), nyuzi za wanyama, mimea (miti) na kitu cho chote chenye uhai au kisicho na uhai kitakachotangazwa katika gazeti la Serikali kuwa ni zao la msitu.

"Mazingira" kama ilivyotafsiriwa katika Sheria ya usimamizi wa Mazingira Na. 20 ya mwaka 2004 yanahusisha maumbile halisi yawazungukao binadamu ikiwa ni pamoja na hewa, ardhi, maji, tabia nchi, sauti, mwanga, harufu, ladha, vijiumbe hali za kibiolojia za wanyama na mimea, rasilimali za kitamaduni na masuala ya uchumi na jamii na inahusisha mazingira asilia na yaliyoundwa na binadamu na jinsi yanavyoingiliana.

"Mfugaji" maana yake ni mtu ye yote anayejishughulisha na ufugaji mifugo katika eneo la Halmashauri.

"Mkurugenzi" maana yake ni Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Mkuranga pamoja na Afisa ye yote wa umma atakayeteuliwa kutekeleza majukumu ya Mkurugenzi.

"Mifugo" maana yake ni mifugo yo yote inayofugwa na binadamu.

"Misitu" maana yake ni eneo la ardhi ambalo limefunikwa angalau kwa asilimia 10 ya miti, uoto wa asili au iliyopandwa, au asilimia 50 au zaidi, ya vichaka na miti na miti inayoota upya ambayo itajumuisha aina yote ya misitu ya hifadhi ambayo itatangazwa chini ya Sheria ya Misitu Na. 14 ya mwaka 2002 na mazao yote ya misitu ikijumuisha majani na nyasi ndani ya eneo la Halmashauri.

"Taka" kama ilivyo katika Sheria ya usimamizi mazingira ya mwaka 2004 maana yake ni kitu cho chote kimiminika, kigumu, gesi na mionzi, kinachotoa harufu mbaya, au kilichohifadhiwa katika mazingira ya hali ya ujazo, uozo au hali nyingine yo yote inayosababisha uharibifu wa mazingira, ambayo inajumuisha taka.

"Taka ngumu" kama ilivyo katika Sheria ya usimamizi mazingira Na. 20 ya mwaka 2004 ni taka ambazo haziko katika umajimaji kutoka majumbani. Katika majengo ya biashara, viwandani na kutoka katika shughuli za kilimo, pamoja na taka za vyakula, karatasi plastic au taka laini zinazotokana na ujenzi au ubomoaji majengo utengenezaji bustani na shughuli za uchimbaji madini, mizoga ya wanyama na mabaki ya magari mabovu (scraps).

"Taka za Viwandani" kama ilivyotafsiriwa katika Sheria ya usimamizi wa Mazingira Na. 20 ya mwaka 2004, maana yake ni Uchafu unaotokana na uzalishaji viwandani au uchafu usiotokana na uzalishaji viwandani ambao ni chanzo cha nishati, maji, mimea iliyotiwa dawa, au mawasiliano, pamoja na taka nyinginezo ngumu kama zilivyotafsiriwa katika Sheria ya Mazingira 2004 sehemu ya IX.

"Uchafu Hatari" kama ilivyotafsiriwa katika Sheria ya Usimamizi wa Mazingira ya mwaka 2004. Maana yake ni kitu cho chote kigumu, chenye majimaji, gesi au taka zitokazo viwandani, au mafuta machafu, ambayo yanaleta athari za kikemia, kwa binadamu au mazingira.

"Uchafu wa Mazingira" kama ilivyo katika Sheria ya usimamizi wa Mazingira Na. 20 ya mwaka 2004 ni mabadiliko ya hali ya hewa ya moja kwa moja au yasiyo moja kwa moja, joto, kemikali, biolojia, au zana za mionzi katika mazingira ambayo zana hizo zinafanyia kazi au kutoa harufu mbaya, mrundikano wa taka ambao unaathiri watumiaji, au unaosababisha hali ya hatari kwa afya ya jamii, usalama, au ustawi au hatari kwa wanyama, ndege, wanyama pori, samaki, au viumbe vyote vya baharini, mimea au kusababisha hali mbaya ya hewa, upungufu, au kizuizi ambacho ni sehemu katika sheria hizi.

"Udongo" kama ilivyo katika Sheria ya Usimamizi wa Mazingira ya mwaka 2004 maana yake ni pamoja na dunia, mchanga, miamba, miamba tope, madini, uoto wa mimea, mimea na wanyama iliyoko chini ya udongo pamoja na vumbi.

"Vitu hatari" maana yake kama ilivyotafsiriwa katika Sheria ya usimamizi wa Mazingira ya mwaka 2004, ni kemikali yo yote, taka gesi, madawa, vidonge, mimea wanyama au viumbe hai visivyoonekana ambavyo ni hatari kwa afya ya binadamu, maisha au mazingira.

"Waziri" maana yake ni waziri mwenye dhamana ya Serikali za Mitaa.

## SEHEMU YA PILI
### MASHARTI YA UFUGAJI

Wajibu wa mfugaji

4. Kila mfugaji chini ya Sheria Ndogo hizi:-

(a) atatakiwa kufuga idadi ya mifugo kama itakavyoamriwa na Halmashauri.

(b) atatakiwa kufuga na kulisha mifugo yake katika maeneo ya malisho yaliyopangwa na Halmashauri.

(c) atatakiwa kupitisha mifugo yake katika njia (stock routes) zilizopangwa na kutengwa na Halmashauri.

(d) atatakiwa kuwa na kadi ya mifugo itakayoonyesha idadi na aina ya mifugo aliyonayo.

(e) atatakiwa kupeleka mifugo katika majosho kama atakavyoagizwa na Halmashauri.

(f) atatakiwa kupeleka mifugo yake katika vituo vya chanjo kama ilivyoamriwa na Halmashauri, na atalipia chanjo hiyo kama atatakiwa kufanya hivyo.

(g) atatakiwa kuchangia gharama za ukarabati wa majosho kama sehemu ya mchango wake, pale itakapobidi kufanya hivyo, na kwa gharama itakayopendekezwa na Halmashauri.

(h) atatakiwa kuchangia gharama za uboreshaji wa maeneo ya malisho yaliyotengwa na Halmashauri.

(i) atatakiwa kuweka alama kwenye mifugo yake (Branding, ear tags) na katika viungo vya mifugo vinavyopendekezwa ili kutoharibu zao la ngozi.

(j) atatakiwa kuhudhuria mafunzo ya ufugaji kama atakavyo hitajiwa na Halmashauri.

(k) kutokata miti kwa lengo la kufukuza mbung'o.

5. Ni marufuku kwa mfugaji ye yote:- Masharti ya mfugaji

(a) Kuchunga, kulisha, au kunywesha maji mifugo katika maeneo ya mipango miji pamoja na maeneo yote ambayo hayakutengwa kwa ajili hiyo.

(b) kusafirisha mifugo kwa kuiswaga barabarani.

(c) kusafirisha au kuhamisha mifugo kutoka eneo moja hadi lingine bila kibali kutoka kwa Halmashauri.

(d) kibali cha kuingiza mifugo katika eneo la Halmashauri kitatolewa na afisa kilimo na mifugo.

(e) kuuza au kununua mifugo katika maeneo ambayo siyo mnada, masoko au maguli ya mifugo yaliyoidhinishwa na Halmashauri.

(f) kufuga mifugo mingi katika eneo dogo la Halmashauri.

(g) Ni marufuku kwa mfugaji ye yote kupitisha mifugo katika maeneo ambayo hayakuidhinishwa na Halmashauri kupitisha mifugo.

6. (1) Halmashauri itakamata mifugo au mfugo wo wote utakaoonekana unazurura hovyo katika eneo la Halmashauri ambapo hapajaruhusiwa kuchungia mifugo. Kudhibiti mifugo inayo-zurura ovyo

(2) Mfugo wo wote utakaokamatwa utalipiwa faini kama itakavyopangwa na Halmashauri na baada ya kulipia gharama hizo mfugaji atarudishiwa mifugo yake.

(3) Endapo mwenye mifugo au mfugo hatatokea ndani ya siku saba (7) tangu kukamatwa kwa mifugo hiyo, Mkurugenzi wa Halmashauri atakuwa na haki ya kuuza kwa mnada mfugo au mifugo hiyo baada ya kupata idhini ya Mahakama.

(4) Baada ya mauzo, Mkurugenzi atakata fedha za faini, gharama za mnada na gharama za ulinzi na fedha zitakazobaki atapewa mwenye mifugo na kama ataonekana ndani ya siku kumi na nne (14) fedha hizo zitaingizwa katika vyanzo vya mapato vya Halmashauri.

(5) Endapo mwenye mifugo hiyo atakuwa na sababu za msingi za kutofika kwake katika muda wa siku kumi na nne (14) halmashauri itarudisha fedha zake.

(6) Endapo kutatokea kufa kwa mifugo au mfugo Halmashauri haitawajibika na ulipaji wa gharama zo zote.

Ukaguzi wa mifugo

7.-(1) Itakuwa halali kwa afisa kilimo na mifugo, maafisa watendaji wa kata na vijiji na Afisa ye yote wa Halmashauri atakayeteuliwa kusimamia utekelezaji wa Sheria Ndogo hizi kuingia katika nyumba au jengo lo lote wakati wo wote kwa madhumuni ya kukagua na kuhesabu idadi ya mifugo iliyomo katika nyumba hiyo.

(2) Mtu ye yote atakayewazuia Maafisa waidhinishwa katika kifungu cha 7(1) kutekeleza wajibu wao chini ya Sheria Ndogo hii atakuwa ametenda kosa.

Wajibu wa Halmashauri

8.-(1) Ni wajibu wa Halmashauri kutenga maeneo maalumu kwa ajili ya shughuli za malisho kwa kuzingatia idadi ya mifugo ndani ya eneo la Halmashauri na kwa mujibu wa Sheria ya Ardhi Sura ya 113 na 114 pamoja na Sheria ya Usimamizi wa Mazingira Na. 20 ya mwaka 2004.

(2) Halmashauri itatenga njia maalumu ya kupitisha mifugo kwenda na kurudi malishoni au Minadani.

(3) Halmashauri itafanya sensa ya mifugo na kutoa kadi za mifugo na elimu ya ufugaji bora kwa jamii.

Taratibu za ufugaji

9.-(1) Wafugaji wote watatakiwa kuzingatia masharti ya kufuga kama yalivyo katika Sheria Ndogo hizi au Sheria yo yote iliyotungwa na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

(2) Kila mfugaji atatakiwa kupeleka mfugo au mifugo yake machinjioni au mahali huduma hiyo inapopatikana na itakuwa ni marufuku kwa mtu ye yote kuchinjia nyama mahali pengine po pote.

(3) Ni marufuku kwa mtu ye yote kununua, kuuza au kufanya Biashara ya kubadilishana aina yo yote ya mifugo katika eneo lo lote la Halmashauri isipokuwa kwenye minada au magulio yaliyotengwa kwa shughuli hiyo.

## SEHEMU YA TATU
### KILIMO NA UHIFADHI WA ARDHI

10.-(1) Mtu atakayetaka kuendesha shughuli za kilimo katika Halmashauri atatakiwa kuzingatia taratibu za kilimo kama zitakavyotolewa na Halmashauri kwa kuzingatia Sheria ya Ardhi sura ya 113 na 114 na Sheria nyingine zitakazotungwa na Bunge. Taratibu za kilimo

(2) Itakuwa halali kwa Afisa kilimo kuingia katika shamba lo lote kwa madhumuni ya kufanya ukaguzi na kuhakikisha utekelezaji wa Sheria Ndogo hizi.

11.-(1) Ni marufuku kwa mtu ye yote kulima katika miteremko, karibu na vyanzo vya maji, kandokando ya mito, mabwawa na maziwa au kufanya jambo lo lote litakaloharibu hifadhi ya mazingira bila kuzingatia ushauri wa Afisa Kilimo. Masharti kwa mkulima

(2) Ni marufuku kwa mtu ye yote kutumia kinyume ardhi iliyotengwa kwa matumizi ya kilimo kama ilivyopangwa na kuidhinishwa na Halmashauri.

(3) Ni marufuku kwa mtu ye yote kusafisha shamba kwa ajili ya kilimo kwa njia ya kuchoma moto isipokuwa kwa kibali maalumu kutoka kwa Halmashauri.

(4) Kibali kitakachotolewa chini ya Sheria Ndogo hizi kitakuwa cha maandishi na kitaonyesha jina la mwenye kibali, tarehe na eneo analotaka kuchoma moto.

(5) Muda unaotakiwa kuchoma moto chini ya Sheria Ndogo hizi ni kuanzia saa 12:00 asubuhi hadi saa 4:00 asubuhi.

(6) Ni wajibu wa Halmashauri kusimamia shughuli za Kilimo na kuhakikisha kuwa wanazuia kilimo cha kuhamahama na kuhimiza Kilimo cha mzunguko (crops rotation).

Uhifadhi wa uoto wa asili

12. Ni wajibu wa wakazi wa eneo ambalo uoto wa asili au mazingira ya eneo husika yameharibiwa, kuhakikisha kuwa wanalirudisha katika hali yake ya kawaida kwa kupanda miti au kutoendelea kuharibu mazingira na kuwezesha uoto urudi katika hali yake.

Uchimbaji mchanga na kokoto

13. Ni marufuku kwa mtu ye yote kuchimba mchanga katika maeneo yasiyoruhusiwa na Halmashauri kama vile katika maeneo ya makazi ya watu, maeneo yaliyohifadhiwa kando kando ya mito au ndani ya mto, bwawa au ziwa isipokuwa kwa ruhusa maalumu ya Halmashauri.

14. Ni marufuku kwa mtu ye yote kujenga nyumba au jengo lo lote katika eneo la hifadhi.

## SEHEMU YA NNE
### HIFADHI YA VYANZO VYA MAJI

Wajibu wa kulinda vyanzo vya maji

15. (1) Halmashauri itawajibika kuanzisha, kusimamia na kulinda vyanzo vya maji.

(2) Halmashauri itachukua hatua kali za kisheria dhidi ya mtu ye yote atakayeharibu chanzo cha maji au kushindwa kushiriki katika shughuli za kuhifadhi vyanzo vya maji bila sababu ya msingi.

Kulinda eneo la hifadhi

16.-(1) Ni marufuku kwa mtu ye yote kulima, kukata miti, kuchunga mifugo katika umbali wa mita 60 toka vyanzo vya maji au kufanya jambo lolote linaloharibu kwa namna yo yote chanzo cha maji na hifadhi ya mazingira.

(2) Itakuwa ni wajibu wa Halmashauri kupanda miti isiyonyonya maji katika vyanzo vya maji kwa kuzingatia maelekezo ya Afisa Misitu.

(3) Ni marufuku kwa mtu ye yote kumiliki eneo la chanzo cha Maji isipokuwa Halmashauri.

17.-(1) Ni marufuku kwa mtu ye yote, kiwanda, Taasisi, Shirika kuelekeza mabomba ya maji machafu kwenye mito, mabwawa, ziwa, visima, mifereji, chemichemi au sehemu yo yote ambayo ni chanzo cha maji kwa ajiili ya matumizi ya binadamu na wanyama au viumbe vingine vilivyo hai. Uchimbaji wa vyanzo vya maj

(2) Ni marufuku mtu ye yote kuweka kitu cho chote chenye sumu ndani ya maji ambayo yanatumiwa na binadamu au kiumbe cho chote hai.

## SEHEMU YA TANO
### HIFADHI YA MISITU

18.-(1) Ni marufuku kwa mtu ye yote kuchoma moto misitu kwa namna yo yote ile katika Misitu iliyoko eneo la Halmashauri. Kuchoma au kusababisha moto

(2) Iwapo moto utatokea katika eneo la Halmashauri, kiongozi wa eneo husika atawajibika kutoa ishara ya hatari kwa kutumia njia iliyozoeleka kuamuru wakazi wa eneo hilo kwenda kuzima moto huo unapoonekana kuwa na madhara kwa maisha, mali za watu na uharibifu wa mazingira katika eneo hilo.

(3) Kila mkazi wa eneo hilo atawajibika kushiriki katika zoezi la kuzima moto huo endapo atatakiwa kufanya hivyo, kama atashindwa kushiriki katika kuzima moto bila sababu ya msingi atakuwa ametenda kosa.

19. Mtu ye yote aliyepata kibali cha kuchoma moto atalazimika kutoa taarifa ya siku saba (7) kabla ya kuchoma moto kwa majirani walioko katika eneo analotaka kuchoma na ataweka njia za kuzuia moto. Kibali kuchom moto

20.-(1) Ni marufuku kwa mtu yo yote kukata miti katika maeneo ya misitu iliyohifadhiwa kwa ajili ya matumizi ya aina yo yote bila kupata kibali kutoka Halmashauri. Ukataji miti

(2) Halmashauri itatakiwa kuhakiki kama miti inayovunwa imekomaa na inafaa kwa ajili ya matumizi.

(3) Ni marufuku kwa mtu ye yote kuvuna miti katika msitu ambao umehifadhiwa kwa ajili ya viumbe maalumu ambao ni rasilimali kwa Taifa.

(4) Watu wanaovuna miti kwa ajili ya kuchoma mkaa watatakiwa kuwa na eneo maalum lililoidhinishwa na Halmashauri kwa ajili ya kuchoma mkaa.

Wajibu wa kupanda miti

21.-(1) Kila Mkazi wa Halmashauri atawajibika:-

(a) kupanda na kutunza miti katika eneo lake;

(b) kupanda na kutunza miti katika makazi yake;

(c) kupanda na kutunza miti katika shamba au mashamba anayomiliki.

22. Kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi kila kijiji:-

(a) kitawajibika kutenga eneo la hifadhi ya Msitu wa asili kwa ajili ya matumizi ya baadaye.

(b) kitalazimika kutunza miti yote inayopandwa katika eneo la Kijiji;

(c) Kitahakikisha ya kuwa kila kaya inapanda miti isiyopungua kumi kwenye eneo la nyumba yake.

(d) Mtu ye yote anayetaka kukata miti au mti wa matumizi ya kuchonga vifaa, kujenga nyumba, kutengeneza zizi na shughuli nyinginezo, itabidi apate kibali cha maandishi toka kwa Mwenyekiti wa Kijiji, Mtendaji wa Kijiji na kibali cha Afisa Maliasili wa Wilaya au Wasaidizi wake kwa miti iliyopandwa na kuhifadhiwa na Halmashauri ya Wilaya.

(e) kila kijiji kitapaswa kutenga na kupanda shamba la miti ekari 2 kila mwaka na kulitunza.

(f) kila Shule au Taasisi nyinginezo Wilayani itapaswa kupanda miti ya kukinga upepo kuzunguka majengo yake na kuwa na shamba lisilopungua miti hekta 2.

(g) kijiji kitapaswa kutunza na kuhifadhi miti na nyasi kwenye milima, makorongo na vyanzo vya maji, ili kuzuia mmomonyoko wa udongo.

(h) kijiji kitahakikisha kuwa kila anayeandaa shamba kwa ajili ya kilimo hatumii moto na anapanda miti kwenye mipaka ya shamba lake kama kinga upepo.

(i) kila mtu mwenye nyumba kwenye Mji mdogo atawajibika kupanda miti kando ya barabara inayopita mbele ya nyumba yake na kuitunza.

(j) kila Mwenyekiti wa Kitongoji, Mtendaji wa Kijiji, Mkuu wa Taasisi yo yote Wilayani atahakikisha kuwa Kijiji au Taasisi ina msitu wa Hifadhi wa miti ya kupandwa au ya asili iliyotengwa kwa madhumuni ya kuhifadhi ardhi, mazingira na matumizi ya baadaye.

## SEHEMU YA SITA
### TAKA NGUMU NA LAINI

23.-(1) Ni wajibu wa Halmashauri kutenga eneo kwa ajili ya kutupa taka ngumu na laini kusimamia kwa karibu usafi katika eneo lake. Utt wa ngu na l

(2) Mtu ye yote atakayetupa ovyo taka ngumu au laini au kujisaidia katika kingo za maziwa, mabwawa au kwenye vyanzo vya maji vilivyoko katika Halmashauri atakuwa ametenda kosa.

24. Ni marufuku kuendesha shughuli za karakana, mashine ya kusaga, kuranda mbao, kukamua maji ya matunda, kuchomelea vyuma au kuendesha shughuli yo yote inayozalisha Uchafu ambao unaleta athari kwa binadamu na viumbe wengi katika maeneo ya makazi ya watu bila kuzingatia taratibu za ujenzi. Uen shaj viwa

## SEHEMU YA SABA
### MAKOSA NA ADHABU

25. Mtu ye yote atakuwa ametenda kosa ikiwa:- Mako yanay husu mifug

(a) ataingiza mifugo katika eneo la Halmashauri bila kibali.

(b) atasafirisha mifugo bila kuwa na kibali.

(c) atalisha mifugo katika maeneo yasiyoruhusiwa.

(d) atafuga mifugo zaidi ya idadi iliyoruhusiwa.

(e) atavua samaki kwa kutumia sumu au nyavu zenye matundu madogo (kokoro).

Makosa yanayohusu kilimo

26. Mtu ye yote atakayekiuka masharti ya kilimo, kuchimba mchanga, kokoto, madini katika maeneo yasiyoruhusiwa na Halmashauri atakuwa ametenda kosa.

Makosa yanayohusu kuhifadhi ardhi

27. Mtu ye yote atakayekiuka masharti ya kuhifadhi Ardhi atakuwa ametenda kosa.

Makosa yanayohusu vyanzo vya maji

28.–(1) Mtu ye yote atakayeharibu vyanzo vya maji au kushindwa kushiriki katika shughuli za kuhifadhi vyanzo vya maji atakuwa ametenda kosa.

(2) Mtu ye yote atakayebainika kuwa ameweka sumu ya aina yo yote kwa namna yo yote ambayo inaathiri maisha ya binadamu na viumbe wengine ambao ni rasilimali ya Taifa atakuwa ametenda kosa.

Makosa yanayohusu kuharibu misitu

29. Mtu ye yote atakuwa ametenda kosa ikiwa:-

(a) atachoma au kusababisha moto katika misitu bila kibali au;

(b) atashindwa kushiriki katika kuzima moto au;

(c) atavuna mazao ya misitu katika misitu iliyohifadhiwa na isiyohifadhiwa bila kibali au;

(d) atachoma mkaa na kukata kuni bila kibali, au

(e) atafyeka nyasi, kung'oa vichaka na kung'oa visiki kwenye misitu bila kibali;

(f) atachoma au kusababisha moto katika misitu bila kibali au:

(g) atavuna mazao ya misitu katika misitu iliyohifadhiwa na isiyohifadhiwa bila kibali au;

(h) atachoma mkaa na kukata kuni bila kibali au;

(i) atafyeka nyasi, kung'oa vichaka na kung'oa visiki kwenye misitu bila kibali;

(j) atachunga mifugo kwenye eneo lo lote lililopandwa miti au iliyohifadhiwa kama bustani ya miti;

(k) atakata miti au kuchungia mifugo kwenye miti iliyopandwa kwa ajili ya kuzuia mmomonyoko wa udongo au kinga upepo;

(l) atabandua magome ya miti kwa ajili ya kutengeneza vilindo, mzinga na vitu vingine bila ya kuwa na kibali;

(m) atalima au kukata miti katika vyanzo vya maji, milima, kando ya njia, makorongo na sehemu nyingine zo zote zinazohifadhiwa ili kupunguza mmomonyoko wa udongo.

Makosa yanayohusu taka ngumu na laini

30. Mtu ye yote atakayetupa ovyo taka ngumu au laini katika maeneo yo yote yasiyoruhusiwa na Sheria Ndogo hizi au Sheria nyingine yo yote iliyotungwa na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania atakuwa ametenda kosa.

Makosa yanayohusu taka za majimaji

31. Mtu ye yote atakayetiririsha maji machafu yanayoleta madhara kwa binadamu na viumbe vingine hai atakuwa ametenda kosa.

Makosa yanayohusu viwanda

32. Mtu ye yote atakayeendesha shughuli za kiwanda au viwanda vidogo, karakana, mashine za kusaga na kukoboa nafaka, mashine za kuranda mbao katika makazi ya watu bila kuzingatia taratibu za mipango miji atakuwa ametenda kosa.

33. Mtu ye yote atakayevunja masharti yaliyowekwa na Sheria Ndogo hizi atakuwa ametenda kosa na akipatikana na hatia atatozwa faini isiyozidi shilingi laki tatu (300,000/-) au kifungo kisichozidi miezi kumi na mbili jela au adhabu zote mbili kwa pamoja yaani faini na kifungo.